# Nipashe

Jumamosi Januari 25, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580137

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## CCM yashtukia mchezo, mbinu za kificho wapinzani uchaguzi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wizara Mambo ya Ndani kaa la moto

• **Miaka** minne mawaziri wanne, tangu uhuru wamepita 27, sababu kuingia na kutoka zabainika... *Endelea ukurasa 2*






Waziri wa Madini, Dotto Biteko na Rais wa kampuni ya Barrick, Dk. Mark Bristow, wakionyesha mikataba baada ya kusaini mbele ya Rais Dk. John Pombe Magufuli, makubaliano ya kuendesha kwa pamoja kampuni mpya ya uchimbaji wa madini ya Twiga, kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya Barrick, Ikulu jijini Dar es Salaam jana, ambapo, Serikali itakuwa na hisa ya asilimia 16, katika kampuni hiyo. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Magufuli aagiza makinikia bandarini Dar kupigwa bei

UKURASA 2

## KCMC yajitosa upandikizaji mbegu za uzazi

UKURASA 3

**MICHEZO** **EYMAEL AONA KITU YANGA VS PRISONS** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Madiwani Chadema wakimbilia CCM

**Na Novatus Makunga,** ARUSHA

IDADI ya madiwani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ambayo inaongoza Halmashauri ya Jiji la Arusha, imeendelea kupukutika baada ya madiwani watatu kujiengua kwa mpigo na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi(CCM).

Sambamba na madiwani hao, pia Katibu wa Chadema Wilaya ya Arusha Mjini, Innocent Kisanyage, ametangaza kujiuzulu na kujiunga na CCM. Wote hao wamedai kuwa wanaunga mkono juhudi za Rais John Magufuli.

Madiwani hao wamejiengua ikiwa ni miezi mitatu tangu aliyekuwa Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha, Calist Lazaro, kuondoka ndani ya chama na baadaye kufuatiwa na madiwani wengine tano mwishoni mwa Novemba, mwaka jana na kujiunga na CCM.

Waliotangaza kujiuzulu juzi na kata zao kwenye mabano ni Melance Kinabo (Themi), Zacharia Mollel (Oloirien) na James Lyatuu wa Unga Limited.

Hatua ya kujiengua kwa madiwani hao imeiporomosha Chadema ambayo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, iliibuka na ushindi hivyo kuwa na madiwani 34 pamoja na mbunge.

Kwa sasa Chadema imebakiwa na madiwani 16 akiwemo Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema na yule wa Viti Maalumu Joyce Mukya, huku CCM ikiwa na madiwani 10 akiwamo Mbunge wa Viti Maalumu, Catherin Magige.

Wakizungumzia sababu za kujiengua Chadema na kuomba kujiunga na CCM, madiwani hao walisema wamechukua hatua hiyo, kwa lengo la kuunga mkono kazi zinazofanywa na Rais Magufuli.

"Mimi sioni 'future' (mustakabali) kwa kesho nikiwa ndani ya Chadema kwenye mpango mzima wa kuleta maendeleo katika Jiji la Arusha na taifa kwa ujumla. Kwa busara na maamuzi (uamuzi) yangu (wangu) nimeamua kuondoka," alisema Kinabo.

Alisema chini ya Rais Magufuli hivi sasa, upelekaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakwenda kwa uwiano sawa na wa kasi kubwa bila ubaguzi wowote. Alisema mipango yote ndani ya Jiji la Arusha imekuwa ikisimamiwa vyema na Mkurugenzi wa Jiji, Dk. Maulid Madeni.

Naye Mollel alisema ameamua kung'atuka ndani ya Chadema ili kuongeza wigo wa fursa za maendeleo katika jiji la Arusha badala ya kuwa kikwazo cha utekelezaji kwa ufanisi.

Lyatuu kwa upande wake alisema amechukua uamuzi huo kwa lengo la kuunga mkono juhudi za maendeleo zinazofanywa na Rais Magufuli katika kutekeleza ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwamo kununua ndege, ujenzi wa treni ya kisasa na mradi wa umeme wa Bonde la Mto Rufiji.

# Wizara Mambo ya Ndani kaa la moto

**Na Sabato Kasika**

WIZARA ya Mambo ya Ndani sasa ni kaa la moto. Ndivyo unavyoweza kuielezea kiurahisi kutokana na namna mawaziri wake wanavyokaa kwa muda mfupi madarakani kisha ama kutumbuliwa au kujiuzulu.

Historia inaonyesha ni mawaziri wawili tu kati ya 27 walioitumikia wizara hiyo kwa kipindi kirefu walau kinachoanzia miaka mitano. Ni Said Maswanya aliyekuwa waziri kwa miaka sita kuanzia mwaka 1967 hadi 1973 na Muhdin Kimario aliyedumu kwa miaka sita pia kuanzia 1983-1989.

Wengi wamekuwa wakiishia mwaka mmoja na baadhi yao kutomaliza hata kipindi cha mwaka mmoja madarakani kisha kuondoshwa au kujiuzulu.

Waziri aliyejiuzulu kwa utashi wake katika wizara hiyo tangu nchi ipate uhuru mwaka 1961 ni Ali Hassan Mwinyi, aliyeteuliwa mwaka 1975 kisha kutangaza kujiuzulu mwaka mmoja baadaye kutokana na kashfa ya mauaji.

Mwaka 1976, akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mwinyi alilazimika kujiuzulu nafasi yake baada ya kutokea mauaji katika mkoa wa Shinyanga, lakini miaka tisa baadaye akawa Rais wa Tanzania kwa kipindi cha miaka 10.

Orodha kamili ya mawaziri katika wizara hiyo tangu uhuru ni Sir George Kahama aliyeiongoza kwa mwaka mmoja kuanzia mwaka 1961 hadi 1962 akifuatwa na Oscar Kambona (1962-1963), Lawi Sijaona (1963-1965) na Job Lusinde (1966-1967).

Kama ilivyodokezwa awali, Maswanya ni miongoni mwa mawaziri wawili waliokaa wizarani hapo kwa muda mrefu zaidi akianzia mwaka 1967 hadi 1973, akifuatwa na Omari Muhaji (1973-1974), Ali Hassan Mwinyi (1975-1976), Hassan Nassoro Moyo (1977-1978), Salmin Amour (1979-1980) na Meja Jenerali Abdalla Said Natepe (1980-1983).

Baada ya Natepe, kilifuata kipindi kingine kirefu cha miaka sita cha Meja Jenerali Muhidini Kimario (1983-1989), Nalaila Kiula (1990), Augustino Mrema (1990-1994), Ernest Nyanda (1994- 1995), Ali Ameiir Mohamed (1995-2000), Muhamed Seif Khatib (2000-2002), Omar Ramadhan Mapuri (2003-2005), John Chiligati (2006).

Wengine ni Joseph Mungai (2006-2008), Lawrence Masha (2008-2010),

Shamsi Vuai Nahodha (2010-2012), Dk. Emmanuel Nchimbi (2012-2013), Mathias Chikawe (2014-2015), Charles Kitwanga (2015-2016), Dk. Mwigulu Nchemba (2016-2018), Kangi Lugola (2018-2020) na sasa George Simbachawene.

**MIAKA 4 MAWAZIRI 4**

Kumekuwa na sababu zinazotofautiana katika kutumbuliwa kwa mawaziri wanaoteuliwa kuiongoza wizara hiyo. Wapo walioondolewa kutokana na kashfa za uonevu dhidi ya wananchi na wengine sababu za kimaadili.

Katika miaka minne ya Rais John Magufuli madarakani, wizara hiyo sasa ina majina ya mawaziri wanne, Alianza na Charles Kitwanga, Mbunge wa Misungwi, aliyetumbuliwa Mei 2016 kutokana na kile kilichoelezwa na Ikulu kuwa aliingia bungeni na kujibu swali lililoelekezwa wizarani kwake akiwa amelewa pombe.

Dk. Mwigulu, aliyekuwa Waziri wa Kilimo kipindi hicho, alikabidhiwa kiti cha Kitwanga lakini miaka miwili baadaye, 2018, akatumbuliwa kutokana na zaidi ya sababu

INAENDELEA UK. 8



Wanafunzi wakivuka barabara kwa tahadhari katika eneo la Kigogo CCM, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# JMP aagiza makinikia kupigwa bei

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameagiza makontena ya mchanga wa dhahabu (makinikia) yaliyozuiwa katika bandari ya Dar es Salaam kwa zaidi ya miaka miwili yauzwe na faida iende kampuni ya ya uchimbaji madini ya Twiga.

Baada ya mgogoro uliodumu tangu mwaka 2017, Kampuni ya Barrick na serikali ziliamua kuunda kampuni ya Twiga ambayo sasa ndiyo itakayosimamia migodi mitatu iliyokuwa chini ya Acacia.

Katika kampuni hiyo, Barrick Gold inamiliki asilimia 84 ya hisa zote na serikali asilimia 16 na faida itakayopatikana itagawanywa asilimia 50 kwa 50.

Rais magufuli aliagiza hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa utiliwaji saini wa mikataba tisa ya makubaliano ya madini baina ya serikali na kampuni ya madini Barrick.

"Huu ni ushindi mkubwa, ninamshukuru Mungu. Ninawahakikishia Barrick na wawekezaji wengine duniani kuwa Tanzania ni eneo sahihi kwa uwekezaji kwa sababu ni nchi tajiri. Ukweli ni kwamba tunataka ushirikiano wa pande zote mbili kunufaika," alisema.

Aliongeza kuwa: "Hicho ndicho walikuwa wanakitaka na makubaliano waliyofikia yamemaliza vita kati ya pande zote mbili na kuanzishwa kwa kampuni ya Twiga. "Ninawahakikishia mnaoendesha kampuni zile makontena ambayo yako bandarini ambayo tuliyashika, mkatafute wabia kwa faida ya kampuni ya Twiga.

"Ndiyo maana nimesema yale makontena ambayo niliyashika yalikuwa yameshauzwa na mteja yupo. Pamoja na stori kwamba yanapelekwa kwenye kuyeyushwa haikuwa kweli yalikuwa yanauzwa na mnunuzi mnamjua na alikuwa ameshalipa asilimia fulani.

"Sasa kama huyo mnunuzi anataka kuja kuyanunua, anunue kwa sababu tunajua faida itakayopatikana ni kwa ajili ya kampuni yote."

Rais Magufuli alisema wale ambao hawakuamini sasa wataamini kwamba ushirikiano wa pamoja ni suluhisho.

"Uendeleze kushirikiana kwa ajili ya faida ya pande zote. Picha iliyoonyeshwa na Mark Bristow (Ofisa Mtendaji

INAENDELEA UK. 8

# Watanzania 22 jela kwa kuzamia 'Sauzi'

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imewahukumu Watanzania 22 waliozamia isivyo halali Afrika Kusini, kwenda jela kutumikia kifungo cha miezi sita baada ya kukiri kutoka nchini bila kufuata taratibu.

Washtakiwa hao ni pamoja na Mzuzuri Mohammed, Mohammed Said, Masoro Musa, Mneke Mehra, Kibila Husein, Ali Hassan, Jamalino Rashid, Abdul Nassoro, Waziru Adam na Said Salum.

Wengine ni, Chuwa Sadick, Salum Kasimum, Macalot Alex, Kayenga Winston, Idali Charles, Ibrahim Mohammed, Jafari Zebra, Omane Fizo, Mbona Edson, Ulembo Azide, Fizo Charles na Mnangwa Rajab.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo aliyesikiliza kesi hiyo.

Alisema mahakama yake inawaona washtakiwa wote ni vijana, nguvu kazi ya Taifa la Tanzania, lakini wameondoka nchini na kuzamia Afrika ya Kusini bila kufuata sheria za Idara ya Uhamiaji.

"Mahakama hii inawatia hatiani kwa kuondoka nchini bila kufuata sheria za Idara ya

INAENDELEA UK 7

# CCM yashtukia mbinu za kificho upinzani

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewataka viongozi wenzake wa chama hicho, wajizatiti kuelekea Uchaguzi Mkuu mwaka huu kwa kuwa wapinzani wao wa sasa siyo wale wa nyuma na wana mikakati ya wazi na ya kificho.

Pia, amesema wapo wanachama waliowapoteza baada ya kunyimwa haki zao na wengine walipotaka kugombea, walivurugwa na kuagiza jambo hilo lisitokee tena.

Akifungua kikao cha viongozi watendaji wa chama na jumuiya zake za mikoa na wilaya, Rais Magufuli aliwataka wasibweteke na kujiamini zaidi na wasibabaishwe na kelele ndogondogo za washindani wao ambao nguvu zao alidai zimekwisha.

"Tujipange tufanye mambo yetu kwa utulivu, kwa uhakika na kwa kisayansi zaidi bila kukurupuka," alisisitiza.

Aliwataka waache kugombana kwa sababu ya nafasi za uongozi hususani kwenye ubunge na udiwani kwa sababu taratibu na kanuni za chama ziko wazi.

"Wakati ukifika utatangaziwa na wenye kuonyesha nia wataonyesha na michakato ya ndani ya chama itatumika.

"Ningetamani mwaka huu tuonyeshe ukomavu wa kisiasa na kidemokrasia ndani ya CCM, tuwaache wale wengine wakurupuke, wagombane na kuvunja taratibu, lakini sisi tukubaliane kwenye kila hatua," alisema.

Aliwaomba viongozi wa wilaya na mkoa wakati wa uchaguzi wasiende na majina mfukoni kwamba huyu ni wa mwenyekiti na huyu wa katibu.

"Saa nyingine unakuta mwenyekiti na katibu wanagombana, maslahi yetu tuyaweke nyuma, tuweke maslahi ya CCM, ndani ya CCM hakuna aliyebosi, sisi wote ni watumishi.

"Tuifuate hii miiko na tusisitize suala la rushwa, ukichagua mla rushwa au mtoa rushwa unakiua chama kwa sababu, akishaingia lazima avune alichokitupa, simamieni haki," aliagiza.

Aliwataka wagombea wasikatwe kwa sababu binafsi kwa kuwa anajua ndani yao wapo wengi wamejiandaa kugombea.

"Leo nina raha sana, kama (Dk.) Bashiru unafikiria lolote baya, hakuna baya shetani ameshindwa, leo ni siku ya raha kukutana hapa chama kikubwa, chama kilichoshika uongozi katika taifa hili," alisema.

Aliongeza kuwa wakati wa vikao vyao vilivyofanyika mkoani Mwanza, walipata fursa kujadiliana na kupeana maelezo kuhusu maandalizi ya ilani ya uchaguzi, mwelekeo wa sera za CCM kwa miaka 10 ijayo.

Alisema kamati ndogo ya ilani imeshaanza vikao vyake, hivyo maandalizi yameshaanza.

"Suala la muhimu katika mchakato wa uchaguzi ni kupima na kutathmini nguvu ya chama chetu na hali kadhalika nguvu za

INAENDELEA UK.8

# KCMC yajitosa upandikizaji mbegu uzazi

**Na Mary Geofrey**

KUTOKANA na kukithiri kwa tatizo la wanawake na wanaume kukosa watoto, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro (KCMC), inatarajia kuanza huduma ya upandikizaji wa mbegu za uzazi.

Pia, imeeleza kuwa kwa sasa inatoa huduma ya ushauri na tiba kwa wenza wenye tatizo hilo katika kliniki yake maalum ya huduma za uzazi.

Hayo yalielezwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Sarah Urasa, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ziara ya maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto katika kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Lengo la kampeni hiyo ni kuangazia mafanikio ya serikali yaliyopatikana katika taasisi hizo kwa miaka minne.

Dk. Urasa alisema kwa sasa wanatoa ushauri na tiba kwa wenza wenye matatizo ya kupata watoto, lakini wanatarajia kuanza kutoa huduma ya upandikizaji mbegu za uzazi za wanaume na uoteshaji wa mayai ya kike.

Alisema lengo ni kusaidia wenza ambao hawana uwezo wa kupata watoto na kwamba wanatarajia kuotesha mayai na mbegu hizo kwa kutumia gesi ya Nitrogen inayozalishwa katika hospitali hiyo.

Alisema kwa sasa wanazalisha mitungi 400 kwa siku ya hewa safi ya Oxygen ya kuwekea wagonjwa wa hospitali hiyo na za jirani na hewa ya Nitrogen kwa ajili ya kuhifadhi sampuli na vioteo vya ngozi na mbegu za uzazi.

"Hewa hii ya Nitrogen tutaitumia kuhifadhi mbegu za kiume tutakazopandikiza kwa wanawake hivi karibuni itakapoanza huduma hii, lakini sehemu nyingine, hewa hii inatumika kwa afya ya wanyama," alisema.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi katika hospitali hiyo, Dk. Benjamin Shayo, alisema nchini takwimu za ongezeko la tatizo hilo zinaonyesha limefika asilimia 10 hadi 15.

Alisema kwa sasa KCMC inatoa huduma ya kliniki mara moja kwa wiki na wanatoa huduma za kuchukua vipimo vya Utrasound, kupima homoni na kutoa huduma za ushauri kwa wenza wanaotafuta watoto.

Alisema huduma hiyo ilianza na watu watano kwa siku hadi kufika watu zaidi ya 10, hali inayoonyesha kuongezeka kwa tatizo.

Dk. Shayo alisema tatizo hilo linawakumba watu wenye umri kuanzia miaka

INAENDELEA UK. 8


Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

**PROJECT COORDINATOR**
**Terms of Reference**

| | |
|---|---|
| Position: | Project Coordinator |
| Deadline: | 31st Jan 2020 |
| Duty of Station: | Arusha |
| Reporting to: | Executive Director |

Purpose of the position: To coordinate implementation of Ardhi Yetu Program II project, the project that is implemented by consortium partners in addressing climate change, and land rights. As such, these Terms of Reference (TOR) describe the background, tasks and deliverables for Project Coordinator to provide related services.

**1. General Overview of the Organization**

The Tanzania Natural Resource Forum is a network organization registered in 2006 as a Non- Governmental Organization, with the aim of promoting the improvement of natural resource governance to achieve more sustainable rural livelihoods and better conservation outcomes. TNRF works for improved natural resources governance by helping to bridge the gap between:

- People's local natural resource management needs and practices, and
- National natural resource management priorities, policies, laws and programs

TNRF seeks to support its members by improving communication, sharing information, promoting collaboration and strengthening collective action. TNRF has a growing membership of more than 3,800 people and organizations, supporting professional staff, and a steering committee drawn from the membership.

TNRF facilitates member-driven 'Working Groups' on key policy and practice issues that are of
direct interest to members. These working groups are very collaborative and provide an opportunity for TNRF's diverse membership to tackle concerns at a range of different levels. There are currently working groups engaged in TNRF's three main thematic areas of forestry, wildlife and rangelands. TNRF communications works at a cross cutting level, producing for example a web-site, weekly e-news, policy briefs in collaboration with partners and participatory film or radio targeted at advocacy. TNRF also successfully engages with other stakeholders in establishing round tables for CSOs, donors, international NGOs and government to discuss emerging issues related to the environment.

**2. Background of the Project**

The Tanzania Natural Resource Forum is implementing a Ardhi Yetu Programm II under Care International funding through Care Tanzania for four years from 2018 to 2021. The project is implemented in collaboration with other two partners, HAKIARDHI and PAIKODEO. TNRF is implementing climate change part of the project in four areas of Kiteto, Iringa rural, Simanjiro and Chemba districts. The project aims at helping community to be adaptive and resilient in climate change. TNRF is looking Project Coordinator who will have the following responsibilities:

**3. Core Responsibilities**

- To strengthen relationships with partners and other stakeholders through planning and implementation of AYP Plus activities
- To lead and coordinate project staff to implement project activities in all district covered by AYP Plus
- To effectively ensure that adequate climate change training is provided to both CSOs partners and to community members
- In collaboration with TNRF project coordinator to collect, analyze monitoring data and produce reports on a monthly basis for the programme.
- To work with Communications Coordinator and Monitoring, Evaluation and Learning officer to establish and maintain a learning and advocacy framework for TNRF interaction with partners and members in
- To support MEL officer to develop and maintain outcome monitoring journals; update and maintain a monitoring database.
- To prepare monthly, quarterly and annual reports for submission to the Executive Director and presentation at regular quarterly staff meetings
- To generate information on issues that come up during program implementation and use them for learning purposes as well as for dissemination
- To facilitate communities and organizations to engage and collaborate with local and central government
- To stimulate dialogue among CSOs partners by finding common ground and looking out for win-win situations
- To facilitate participation, information sharing and networking among CSOs and other stakeholders on land rights and climate change issues
- To effectively coordinate representation of small holders' farmers and pastoralists interests at local and national and regional levels
- Coordinate various researches and studies
- To manage all LBI projects and meetings at TNRF.
- Any other assignments assigned by Executive Director

**5. Required qualifications and experience**

The coordinator will have the following broad skill-set and attributes: -

- Bachelor degree in law, natural resource management, Community/rural Development). or in any social science discipline. Advanced degree will be an added advantage.
- Skilled in the use of a range of monitoring tools to improve the strategies for achieving outcomes and for improving performance – experience in outcome monitoring or willingness to learn methodologies
- Skilled in training and participatory learning methodologies, preferably with small holder farmer and pastoral communities
- A thorough knowledge of Logical Framework Analysis and knowledge of Organizational Development Issues
- Strong research, analytical, and writing skills is required.
- Ability to work with consultants, develop Terms of References (ToR) and ensure best long-term outcomes from consultants' work
- Proven knowledge of arrangement and procedures of formal and informal institutions in small holder and pastoral communities
- Experiences not less than 5 years working with climate change related progress, Civil Society organizations, private sectors or community groups, and local government institutions in Tanzania
- Excellent English and Kiswahili (speaking and writing)
- Computer literate in Microsoft office package

**6. Terms of Contract**

This is a project funded position for which a full and attractive package commensurate with the nature of the position will be offered per annual basis, renewable on the basis of performance and availability of funds

**How to Apply:** Interested Candidates for this job are kindly requested to send their CV accompanied by a cover letter to recruitment@tnrf.org, or P.O. Box 15605 Arusha, Tanzania

**Women and youths are encouraged to apply.**

**For details visit:**
**https://www.tnrf.org/en/content/project-coordinator-1**

215598502

# MO Dewji uso kwa uso na Rais wa Ufaransa

**Na Mwandishi Wetu**

MOHAMED Dewji alikuwa Mtanzania na Ofisa Mtendaji Mkuu pekee kutoka Afrika Mashariki aliyealikwa kushiriki dhifa iliyoandaliwa na Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa mjini Paris mwanzoni mwa wiki.

Katika majadiliano, Dewji alikuwa miongoni mwa watu watano waliopata fursa ya kuuliza swali kwa Rais Macron katika ukumbi uliokuwa na maofisa watendaji wakuu zaidi ya 200 kutoka maeneo mbalimbali duniani.

Dewji aliuliza: 'What is your strategy for Anglophone Africa?' (Una mkakati gani kwa nchi za Afrika zinazoongea Kiingereza?). Alizingatia kwamba Ufaransa imejikita kwenye kutoa misaada ya kibiashara na kuimarisha uhusiano wa kisiasa na nchi za Afrika ilizozitawala na zinazoongea Kifaransa).

Macron alijibu kwa shauku akieleza kuwa mikakati ya nchi yake kwa sasa barani Afrika haijikiti tu kwa nchi zinazozungumza Kifaransa. Alisema ushirikiano wao na Rwanda inayoongozwa na Rais Paul Kagame, ni mfano mzuri wa suala hilo.

Baada ya dhifa hiyo, Dewji, miongoni mwa mabilionea vijana barani Afrika, alitumia ukursa wake wa Twitter kuelezea furaha yake ya kukutana na kupata fursa ya kuzungumza na Rais huyo, akisema:

"Nimefurahi kualikwa kwa chakula cha jioni na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron. Uaminifu wake na ufahamu mzuri juu ya mazingira yanayobadilika ya jiografia na ugumu wa kuzunguka uhuru wa kitaifa, kweli vilinigusa! Kiongozi mwenye huruma sana na shauku ya kuona Ufaransa inasonga mbele!"

# Udom yataja sababu mwanafunzi wake kushikiliwa kituo cha polisi

**Na Mwandishi wetu,**
DODOMA

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Faustine Bee, amesema Jeshi la Polisi Mkoani Dodoma, linamchunguza mwanafunzi wa chuo hicho, Masumbuko Juma, kwa tuhuma zinazomkabili ili taratibu nyingine za chuo zifuate kulingana na sheria za nchi na kanuni za chuo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Prof. Bee, mwanafunzi huyo alishikiliwa kwa siku chache na Jeshi la Polisi, lakini amepata dhamana.

Prof. Bee alisema mwanafunzi huyo anasoma Shahada ya Sayansi katika Fizikia mwaka wa tatu na ni mnufaika wa mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa asilimia 100.

"Mwanafunzi huyo alishikiliwa na Jeshi la Polisi kwa siku moja Januari 22 hadi 23 mwaka huu na baadaye kutolewa kwa dhamana," alisema.

Alieleza kuwa Masumbuko anatuhumiwa kwa kutenda makosa matatu tofauti ya kimtandao ambayo hayana uhusiano na tatizo la ukosefu wa maji ambalo hata hivyo alidai lilishatatuliwa na kutolewa ufafanuzi na ofisi hiyo kupitia taarifa ya Januari 20 mwaka huu.

Alisema tuhuma tatu zinazomkabili mwanafunzi huyo zinaendelea kuchunguzwa na jeshi hilo.

Januari 20 mwaka huu, Prof. Bee alitoa taarifa kwa vyombo vya habari akizungumzia tatizo la ukosefu wa maji kuanzia Januari 12 hadi 19 mwaka huu, lililosababishwa na kuchomoka kwa bomba kubwa la Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira jijini Dodoma (Duwasa) linalosambaza maji eneo la Makulu, Udom na maeneo mengine yanayozunguka chuo.

Alifafanua kuwa bomba hilo lilichomoka kufuatia mvua kubwa inayoendelea kunyesha, hivyo tatizo halikuwa limeikumba Udom peke yake bali na maeneo mengine.

Alieleza kuwa katika siku za ukosefu wa huduma hiyo, chuo kwa kushirikiana na Duwasa, walitumia magari maalum kutafuta maji na kuwapelekea wanafunzi huduma hiyo.



Wanachama wa CCM wakimshangilia Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Rais Dk. John Pombe Magufuli (hayupo), alipokuwa akiwahutubia katika kikao cha Viongozi na Watendaji wa Chama na Jumuiya zake za mikoa na wilaya, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Makusanyo kiduchu ardhi yamchefua Naibu Waziri

**Na Mwandishi Wetu, SUMBAWANGA**

MAKUSANYO kidogo ya kodi ya pango la ardhi katika halmashauri za Mkoa wa Rukwa, yamemkera Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, baada ya kuelezwa kuwa hadi kufikia Desemba 2019, jumla ya Sh. milioni 148.2 zilikusanywa na halmashauri zote nne, sawa na asilimia 7.9.

Akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika mkoa huo jana, Dk. Mabula alikutana na alikutana na watumishi wa sekta ya ardhi na kushangazwa na namna maofisa ardhi wa halmashauri hizo wasivyofuatilia makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kiasi cha kuzifanya halmashauri hizo kukusanya kiasi kidogo cha fedha.

Alisema haiwezekani ndani ya miezi sita halmashauri nne za Mkoa wa Rukwa zikusanye asilimia 7.9 ya kodi ya pango la ardhi, akisisitiza kuwa inatia shaka kama halmashauri hizo zitafikisha hata asilimia hamsini ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020.

Kwa mujibu wa taarifa ya mkoa huo iliyosomwa na Mrasimu Ramani wa Mkoa wa Rukwa, Kelvin Maungi, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, halmashauri za mkoa huo zilikadiriwa kukusanya jumla ya Sh. bilioni 1.88.

Maungi alisema Manispaa ya Sumbawanga ilikusanya kiasi cha Sh. 94,253,273, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi Sh. 16,494,189, Kalambo Sh 1,793,550 na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Sh. 35,680,575 na hadi hadi Desemba 2019, jumla ya Sh. 148,221,587 zilikuwa zimekusanywa kwa halmashauri zote, sawa na asilimia 7.9.

"Wakurugenzi wako 'busy' na masuala mengine, mkoa mzima una asilimia 7.9 ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi, ni aibu na hamuwezi kufikia asilimia 50 ya makusanyo, naagiza wote mkafanye uhakiki wa wadaiwa wa kodi ya ardhi na muwapelekee ilani ili watakaokaidi, wafikishwe kwenye mabaraza ya ardhi," aliagiza.

Naibu Waziri huyo aliagiza kufikia Machi mwaka huu, lazima kuwe na mabadiliko ya utendaji kazi kwenye sekta ya ardhi kwa halmashauri za mkoa huo, vinginevyo atafikiria kama wakuu wa idara wanatosha kuendelea na nafasi zao.

Dk. Mabula alisema mikoa yote aliyoitembelea kwenye ziara zake za kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi, imefikisha au kuvuka asilimia 30 ya makusanyo ya kodi ya ardhi, lakini Mkoa wa Rukwa umemsononesha.

Aliwamwagiza Kamishna wa Ardhi Msaidizi Kanda, Thadei Kabonge, kutoa maelezo kuhusiana na utendaji kazi wa wakuu wa idara kama wanafaa kushika nafasi zao.

Alisema taarifa zilizokuwa kwenye mfumo wa kielektroniki zinaonyesha Manispaa ya Sumbawanga ilitakiwa kukusanya Sh. bilioni 6.7, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Sh. milioni 20, Kalambo Sh. milioni 1.6 na Nkasi Sh. milioni 16 kutokana na halmashauri hizo kuwa na malimbikizo ya wadaiwa kodi ya pango la ardhi.

HABARI KITAIFA

# Waziri amulika gharama upimaji saratani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameagiza Hospitali ya Benjamin Mkapa kupunguza gharama za kuchunguza saratani ya matiti kwa wanawake kutoka Sh. 70,000 hadi 30,0000 kama ilivyo kwa hospitali zingine za taifa.

Pia, ameitaka hospitali hiyo kujiunga na tiba mtandao ili kutoa tiba kwa wagonjwa kwa haraka na kwa ufanisi na kuwapunguzia wagonjwa muda wa kusubiri majibu hususani ya mionzi.

Aliitoa maagizo hayo jana alipotembelea hospitali hiyo kujionea hali ya utoaji huduma. Alisema ni vyema wakajiunga na huduma ya tiba mtandao ili kutoa huduma kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

"Mnatakiwa mkajifunze huduma hii kutoka Hospitali ya Muhimbili au MOI," alisema. Waziri huyo alisema hivi sasa kwenye hospitali nyingi kuna shida ya wataalamu wa kusoma picha kwa kuwa wataalamu wengi waliopo ni wale wa kupiga. "Tunao wataalamu wengi wa kupiga picha maana kwenye mionzi kuna aina mbili za wataalamu -- wapo wa kupiga picha (radiographer) na wa kusoma picha, hivyo serikali itahakikisha inapata wataalamu wengi zaidi wa kusoma ili kukidhi mahitaji," aliahidi.

Waziri Ummy alisema wizara ina lengo la kuziunganisha hospitali za wilaya pamoja na vituo vya afya kwenye mfumo wa hospitali za rufaa za mikoa kwa kufunga senta zitakazosaidia hospitali za wilaya na vituo vya afya vinavyofanya vipimo vya 'utra sound' na 'x-ray' na majibu yakasomwa haraka na wataalamu wa hospitali za rufaa na kutoa majibu haraka bila kumsubirisha mgonjwa kwa muda mrefu.

Alitoa wito kwa wananchi wa Dodoma na mikoa jirani kutosafiri hadi Dar es salaam kupata huduma za kibingwa kwa kuwa huduma zote karibu zinapatikana hapo na wizara itapeleka madaktari bingwa wa mishipa ya fahamu na mifupa.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mwanasha Tumbo (kulia), akitoa maelekezo, alipotembelea kukagua ujenzi Shule ya Msingi Mwarimba, Kata ya Misozwe juzi. Kushoto ni Diwani wa Kata hiyo, Jestina Mntangi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ofisa Mtendaji kizimbani tuhuma kuomba rushwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Ruvuma, imewafikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Tunduru, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Majimaji wilayani humo, Chriss Watson Mwambungu na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Chalinze katika kata hiyo, Emmanuel Mhimba, wakituhumiwa kuomba rushwa.

**Inadaiwa maofisa hao waliomba rushwa hiyo ili wasimfikishe kituo cha polisi mke wa Rombola ambaye alikuwa amekamatwa kwa tuhuma za kuuza gongo.**

Mkuu wa Takukuru mkoani Ruvuma, Yustina Chagaka, aliiambia Nipashe jana mchana kuwa watuhumiwa hao, wakiwa watumishi wa umma, kwa pamoja Novemba 30, mwaka jana, katika Kijiji cha Chalinze, wanadaiwa kuomba hongo ya Sh. 200,000 na kupokea kiasi cha Sh. 100,000 kutoka kwa Simon Rombola.

Inadaiwa maofisa hao waliomba rushwa hiyo ili wasimfikishe kituo cha polisi mke wa Rombola ambaye alikuwa amekamatwa kwa tuhuma za kuuza gongo.

Chagaka pia alidai kuwa siku hiyo hiyo, Mhimba na Mwambungu walidaiwa kuomba hongo ya Sh. 200,000 na baadaye walipokea Sh. 40,000 kutoka kwa Thomas Lukas ili wamsaidie baba yake, Abbas Mohamed Matapata, asifikishwe kituo cha polisi baada ya kukamatwa akiwa anauza pombe haramu aina ya gongo.

Alisema Takukuru inaendelea kufanya kazi kwa weledi na kuwa na mafanikio makubwa, akibainisha kuwa kesi zinazoendelea mahakamani sasa zimefika 12 baada ya mbili mpya kufunguliwa wilayani Tunduru.

Alisema washitakiwa wanatoka katika idara za elimu, Jeshi la Polisi, Maji, Mifugo na Uvuvi na serikali ya kijiji.

# NHC yabanwa ujenzi nyumba

**Na Mwandishi Wetu,** SUMBAWANGA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kuhakikisha inakamilisha mradi wake wa ujenzi wa nyumba za makazi za Jangwani katika Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa mwaka huu wa fedha.

Akizungumza wakati akikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa nyumba hizo za makazi wenye nyumba 20 za ghorofa moja jana katika Manispaa ya Sumbawanga, Dk. Mabula alisema mradi huo lazima ukamilishwe mapema kwa kuwa fedha iliyotumika ni nyingi.

Alitoa maagizo hayo baada ya kuelezwa na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, kuwa mradi huo umekuwa ukimsumbua kutokana na kuchukua muda mrefu bila kukamilika na hivyo kuufanya mkoa kutojua hatma yake wakati uhitaji wa nyumba za kupanga katika Manispaa ya Sumbawanga ni mkubwa.

"Naungana na RC (Mkuu wa Mkoa) kuwa mradi huu umechukua muda mrefu, hivyo ni lazima uishe katika mwaka huu wa fedha wa kiserikali na Aprili mwaka huu, narudi hapa Sumbawanga," alionya.

Kwa mujibu wa Meneja Mawasiliano wa NHC, Muungano Saguya, mradi huo wa ujenzi wa nyumba za makazi Jangwani ulianza Juni 2014 na ulisimama kupisha uchunguzi baada ya kuwapo tuhuma za ubadhilifu kwenye mradi huo.

Hata hivyo, Saguya alisema kiasi cha Sh. milioni 366.2 kinahitahika kumalizia mradi huo na tayari shirika lake limejipanga kwa maandalizi ya ukamilishaji wa mradi na muda wowote umaliziaji nyumba hizo utaanza.

Tayari nyumba moja ya mradi huo ilishanunuliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHF), na ukikamilika, nyumba zake zitapangishwa na kuliingizia shirika Sh. milioni 5.4 kwa mwezi.


## KUMBUKUMBU



**Dr. Tukundonda Simalike Kyando**

Ni miaka sita (6)sasa tangu ulipotangulia katika makazi yako ya milele siku ile ya huzuni ya 25, January 2014. Tunakumbuka kwa upendo na uongozi wako katika familia. Miongozo na mapenzi makubwa uliyotupa ndio yanayotuwezesha kusimama mpaka leo.

Unakumbukwa sana na mke wako Yokebeth K. Kyando, watoto wako wapenzi na wajukuu, ndugu, jamaa na marafiki wote.

**"Bwana akupatie pumziko la milele, na mwanga wa milele akuangazie, upumzike kwa amani."**

**"Bwana alitoa na bwana alitwaa. Jina lake lihimidiwe milele, Amen"**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji Tanzania sasa wajitazame kwa Samatta

**WIKI** hii nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania, Mbwana Samatta aliandika rekodi mpya kwa soka la nchi hii baada ya kuwa Mtanzania wa kwanza kusajiliwa na klabu ya Ligi Kuu England.

Samatta amejiunga na klabu ya Aston Villa akitokea KRC Genk ya Ubelgiji kwa pauni milioni 10 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 29 za Tanzania na tayari amekabidhiwa jezi namba 20 atakayoivaa msimu huu katika timu hiyo iliyopo nafasi ya 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England baada ya kushuka dimbani mara 24 na kujikusanyia alama 25.

Juhudi, kujituma, nidhamu na malengo ndicho tunachoweza kusema kimemsaidia Samatta kufika hapo alipo kwani kwa muda mrefu alishaeleza dhamira yake ya kucheza ligi hiyo inayoongoza kwa kupendwa zaidi duniani.

Samatta ambaye hadi anaondoka Genk ameifungia jumla ya mabao 76 katika mechi 191 alizoichezea, huku msimu huu pekee akiiachia mabao 10 kati ya hayo, alionyesha nidhamu nje na ndani ya uwanja kwa kujituma zaidi tangu akiwa African Lyon, Simba, TP Mazembe ya DR Congo na hatimaye Genk na sasa amefikia malengo yake kwa kwenda kucheza England.

Nipashe tuna kila sababu ya kumpongeza Samatta kwa kuwa mvumilivu, kujituma na hatimaye kufikia malengo yake hayo, ambayo sasa si tu kwamba yanaileteа sifa Tanzania bali pia yataiingizia fedha nyingi za kigeni kwa uwapo wake nchini humo.

Tunasema hivyo, kwa sababu tunafahamu atakuwa balozi mzuri wa taifa letu, hivyo wapo wachezaji wengi, viongozi wa soka na hata mashabiki wake watapenda kuja kuitembelea Tanzania ili kuifahamu nchi anayotoka Samatta, hivyo kulingizia taifa fedha za kigeni.

Lakini pia, fedha atakazolipwa Samatta kwa namna moja ama nyingine moja kwa moja zitasaidia nchi kuingiza fedha za kigeni, jambo ambalo tunapenda kuona wachezaji wengi zaidi wakipata nafasi hiyo ya kucheza soka la kulipwa na si tu Uingereza, bali nchi mbalimbali barani Ulaya.

Tumevutiwa sana na juhudi za Samatta ambaye amenunuliwa na kwenda kuingia timu hiyo ya Ligi Kuu moja kwa moja pasipo kupitia hatua ya majaribio kama ambavyo baadhi ya wachezaji kutoka nchini wamekuwa wakipitia na wengine kushindwa.

Tunakumbuka mwaka 2009, Mrisho Ngassa alipata nafasi ya kwenda kufanya majaribio West Ham wakati huo ikinolewa na Mtaliano Gianfranco Zola, na winga huyo kutakiwa kurejea nchini kujenga mwili zaidi, lakini aliporejea hakufanya kama alivyoelekezwa. Kadhalika, pamoja na kipaji kikubwa alicho nacho kiungo wa zamani wa Simba, kwa sasa Singida United, Haruna Moshi 'Boban' hatujui hadi leo nini kilimkimbiza kucheza soka la kulipwa Sweden.

Si Ngassa na Boban pekee, bali kuna mifano mingi ya wachezaji ambao walishindwa kuonyesha juhudi, kujituma na nidhamu kama ambavyo ameonyesha Samatta na kuweza kufikia malengo yake.


Tunaamini mafanikio hayo ya Samatta sasa yatakuwa kioo cha wachezaji wa Tanzania kuweza kujitazama na kuwa na wivu wa maendeleo ili kufikia malengo yao jambo ambalo litageuza nchi yetu kuwa soko la wachezaji Ulaya.

Lengo letu ni kuona wachezaji wengi wakienda kucheza soka la kulipwa Ulaya, kwa kuwa tunatambua mbali na kuiingizia nchi fedha za kigeni, lakini pia ipo faida kubwa kwa timu yetu ya Taifa, Taifa Stars kuweza kufanya vizuri kwenye mechi za kimataifa.

Hakuna asiyejua kuwa moja ya sababu ya Tanzania kushindwa kufurukuta kwenye michuano ya kimataifa ni kutokana na kutokuwa na nyota wengi waocheza soka la kulipwa ambao wanakuwa na vitu vingi vya ziada vitakavyoweza kumrahisishia kocha kuiunganisha timu.

Hivyo, ni wakati sasa kwa wachezaji wa Tanzania kuonyesha nidhamu kwa makocha, viongozi wa klabu na kujituma zaidi huku wakiwa na malengo ya kufika ama kupita mafanikio aliyoyapata Samatta, hilo likifanyika, hakika kila mmoja atalinyooshea kidole soka letu, lakini pia tunamtaka nahodha huyo wa Taifa Stars asiridhike na alipofika bali alenge kufika mbali zaidi ya hapo kwa kuwa mfungaji bora wa ligi hiyo na hata kucheza klabu kubwa zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Aliye juu yu juu

Na Barnabas Maro

**HALAHALA** Yanga, mgwizi haliwi na funo. 'Mgwizi' ni mnyama anayewagwia au kuwakamata wanyama wengine. 'Funo' ni mnyama anayefanana na paa.

Aliye juu huwa yuko juu ni kama ilivyo, kwa mnyama anayewala wengine kama simba; hawezi kuliwa na funo. Methali hii hutumiwa hasa pale mtu ameshindwa kupambana na mwingine kwa kuwa ana uwezo kumzidi.

Mpaka nilipokuwa naandika makala haya jana Ijumaa, Klabu ya Simba ndio ilikuwa ikiziongoza timu zingine 19 zinazoshiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwa kuwa na alama 41 baada ya kucheza michezo 16 ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu inayoendelea sasa.

Katika michezo hiyo imeshinda mechi 13, imekwenda sare michezo miwili na kuwa timu pekee iliyopoteza mchezo mmoja tu. Aidha, ni timu inayoongoza kwa kufunga mabao 35 na kufungwa idadi ndogo zaidi, yaani mabao saba.

Hata ukitoa mabao saba iliyofungwa kati ya iliyofunga, bado itakuwa ikiziongoza timu zote 19 kwa kufunga mabao 28. Simba inastahiki kupewa kongole (asante).

Napata wazo la kutumia methali isemayo "Angurumapo simba mcheza ni nani?" Maana yake ni mnyama gani anayeweza kucheza anapongurumа simba aliye mfalme wa nyika?

Methali hii huweza kutumiwa kuwapigia mfano watu wanaomdharau kiongozi au mkubwa, lakini wanaojikunyata mara atokeapo. Naam, angurumapo simba mcheza ni nani?

Simba ninayoizungumzia si simba mnyama, bali ni timu ya Simba inayonufaika kwa uwekezaji wa bilionea wao, MO Dewji anayoitoa kizani na kuifanya ya kimataifa. Anayebisha na abishe, lakini ukweli ndio huo.

Kwa hatua waliyofikia Simba, maarufu kwa jina la 'Wana wa Msimbazi,' nawapa kongole ila wasivimbe vichwa kwani ligi ndo kwanza imeanza hivyo lolote laweza kutokea kwani mpira unadunda na kudundika.

Yanga, ambayo mimi ni mwanachama kindakindaki (halisi), naipa moyo kwa methali isemayo: "Anayetafuta hachoki, akichoka keshapata." Maana yake mtu anayetafuta kitu (kwa muktadha huu ubingwa), hachoki kutafuta hadi akipatapo.

Methali hii hutumiwa kumhimiza mtu anayefanya jambo fulani na anayeelekea kukata tamaa kumshauri asikate tamaa.

Wachezaji wa Yanga wanapaswa kutambua kuwa huu ni mzunguko wa kwanza na kuna mwingine wa pili unaoitwa 'lala salama' kwa hiyo hawana sababu ya kukata tamaa kwani penye nia pana njia.

Ilisemwa na wahenga kuwa "Aliye juu mngoje chini." Maana yake aliye juu kama mpanda ngazi hakosi atateremka chini.

Mpaka Alhamisi iliyopita, Yanga ilikuwa nafasi ya nne ikitanguliwa na Simba na Azam FC na 'Wagosi wa Kaya' Coastal Union ya jijini Tanga. Kwa msimamo huo, Yanga (timu ya wananchi) inazitangulia timu 16 ikiwa imecheza michezo 15.

Timu zilizofungwa mabao mengi mpaka Alhamisi iliyopita ni Mbeya City (mabao 24), Singida United 23, Alliance FC (22), Lipuli FC (20), KMC FC (19), Mbao FC na Ruvu Shooting (18).

Kagera Sugar, JKT Tanzania na Ndanda FC zimefungwa mabao 17 kila moja zikifuatiwa na Yanga, Namungo FC, Polisi Tanzania, Mtibwa Sugar na Mwadui FC zilizofungwa mabao 15 kila moja.

Ndanda FC ipo mkiani ikizibeba timu 19 kwa kufunga mabao sita na kufungwa 18 ikiwa na alama tisa.

Wanaozusha kuwa vipigo viwili mfululizo dhidi ya 'timu ya wananchi' (Yanga) kuwa kuna 'mkono wa mtu' wakimnyooshea kidole Charles Boniface eti anahusika na vipigo hivyo, ni wajinga na wambea wanaotaka kuleta vurugu klabuni.

Hakuna timu yoyote ya kandanda duniani isiyofungika wala hakuna inayoweza kuzitawala zingine zote daima. Kadhalika, hakuna timu inayocheza ili ishindwe; kama ipo humu nchini, ipigwe faini kubwa na kuondoshwa kwenye Ligi Kuu sawia (kwa wakati mmoja).

Jambo linalokera ni timu zetu kuruhusiwa kusajili wachezaji wengi kutoka nje ya Tanzania. Jambo hilo linasababisha wachezaji wetu kutopata nafasi ya kuonesha uwezo wao ndani na nje ya nchi.

Baadhi ya wachezaji wa kigeni wanaosajiliwa, ama hawatofautiani na wachezaji wetu au wanapitwa kiuchezaji.

Inaleta picha gani kama timu ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara inachezesha wachezaji saba wa kigeni ilhali wanne tu ndio wazalendo? Maana yake ni kwamba Tanzania hakuna wachezaji wanaofaa! Si kweli wala haiwezekani.

"Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine.

Twafunzwa kuvitegemea vitu vyetu (kwa muktadha huu wachezaji wazalendo) wala si wageni wanaokuja kuchumia kwetu na kwenda kula kwao!

# Mpango kabambe mjini Tunduma wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDUMA



NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (pichani), amezindua mpango kabambe wa miaka 20 (2015-2035) wa Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

Vilevile, amezitaka halmashauri zote nchini ambazo hazijaadaa mipango kabambe katika miji yakle, kufanya hivyo ili kuongeza kasi ya kupanga na kupima miji yote nchini.

Dk. Mabula alizindua mpango huo jana katika mji huo wilayani Momba wakati akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kukagua utekelezaji wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Alisema kukamilika kwa mpango kabambe wa Mji wa Tunduma kumekuja wakati mwafaka kwa kuwa mpango huo utachochea utumiaji fursa na rasilimali zilizoko Tunduma na kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi sambamba na kupunguza au kumaliza migogoro ya ardhi.

"Mpango huu utachochea utekelezaji wa malengo ya muda mrefu ya serikali ya kuwa na uchumi wa kati wa viwanda na hii inajidhihirisha katika mpango kabambe wa Mji wa Tunduma pale jumla ya hekta 4,190, sawa na asilimia 10 ya maeneo yaliyopangwa kwa matumizi ya ardhi, zimetengwa kwa ajili ya viwanda," alisifu.

Alitoa wito kwa halmashauri na wadau wa maendeleo katika Mji wa Tunduma kuandaa mkakati wa mpango kazi wa utekelezaji mpango kabambe sambamba na kutafuta wabia na wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye sekta mbalimbali zilizoainishwa katika mpango huo.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali mstaafu Nicodemus Mwangela, alisema mpango huo ni muhimu kwa mji huo kwa kuwa uko mpakani na una shughuli nyingi huku asilimia 70 ya mizigo ikipitia katika mji huo.

Alisema Mji wa Tunduma unahitaji kutazamwa kwa macho mawili kwa kuwa mwingiliano wa wananchi wa Tanzania na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ni mwingi na kusisitiza katika mkoa wake, Mji wa Tunduma ni wa kwanza kuandaa mpango kabambe huo.

Akielezea mpango huo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Momba, Mary Marcko, alisema, lengo la mpango huo ni kuwa kitovu cha biashara kwenye Mkoa wa Songwe, Nyanda za Juu Kusini na nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara na kutaja maeneo ya kimkakati kuwa ni katikati ya Mji wa Tunduma, miji ndani ya mji, ukanda maalum wa kibiashara na ukanda wa viwanda.

Kwa mujibu wa Katibu Tawala wa Wilaya ya Momba, jumla ya miradi 24 itatekelezwa katika awamu ya kwanza (2015-2020) na kuitaja baadhi yake kuwa ni Kituo cha Mabasi cha Mpemba ambacho ujenzi wake umeanza.

Pia, barabara ya lami kutoka Mpemba hadi Isongole itakayounganisha eneo la Mpemba na nchi jirani ya Malawi kupitia Isongole (Ileje), ujenzi wa hospitali ya Mji wa Tunduma na ukamilishaji ujenzi wa miundombinu ya maji pamoja na ujenzi wa maegesho ya malori unaojengwa katika Kata ya Chapwa.

# Watanzania 22 jela kwa kuzamia 'Sauzi'

INATOKA UK. 3

Uhamiaji, mtakwenda jela kutumikia kifungo cha miezi sita, mmeliingizia gharama taifa kwa kukodi ndege ya kuwarudisha nchini wakati fedha hizo zingeweza kujenga hospitali na kufanya shughuli nyingine za maendeleo," alisema.

Hakimu alisema washtakiwa watakwenda jela kutumikia adhabu hiyo pamoja na kufanya kazi mbalimbali watakazopangiwa na magereza.

Kabla ya kutolewa kwa adhabu hiyo, Wakili wa Serikali, Shija Sitta, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa washtakiwa ili iwe fundisho kwa vijana wengine.

Alidai taratibu za kusafiri nje ya nchi zipo na kwamba hakuna msingi wa watu kwenda Afrika Kusini bila kibali, kitendo ambacho kimedhalilisha taifa kwa kuonekana ni wahamiaji haramu.

Washtakiwa hao kwa nyakati tofauti waliiomba mahakama iwapunguzie adhabu ili kulitumikia taifa.

Awali, akisoma mashtaka, Sitta alidai washtakiwa hao walitoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinyume cha Kanuni za Uhamiaji namba 20(3)(a) G.N namba 657 ya mwaka 1997 inayosomwa pamoja na kifungu namba 48(2) cha Sheria ya Uhamiaji namba 54 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016.

Alidai Januari 21, mwaka huu, maeneo ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), washtakiwa hao, wakiwa raia wa Tanzania, walikutwa wakiwa wametoka nje ya nchi bila kufuata utaratibu wa kutoka nchini kwenda Afrika Kusini kwa kupitia mipaka inayojulikana.

Washtakiwa wote walikubali mashtaka hayo na upande wa mashitaka uliwasomea maelezo ya awali ambapo alidai tarehe zisizofahamika, walitoka Tanzania na kuingia Afrika Kusini bila kufuata taratibu.

Ngwijo alidai katika tarehe hiyo, washtakiwa walikamatwa Afrika Kusini na kuletwa Tanzania na kwamba walifikishwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na kupelekwa Ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam na kuchukuliwa maelezo.

Hata hivyo, washtakiwa wengine 20 walifikishwa mahakamani hapo, lakini hawakusomewa mashtaka kutokana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Agustina Mbando aliyepangiwa kesi hiyo, kupata dharura hivyo kesi hiyo iliahirishwa hadi Jumatatu (Januari 27, mwaka huu).


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
TANZANIA COMMUNICATIONS REGULATORY AUTHORITY

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAHADHARI KWA UMMA

**NDUGU WATANZANIA;**

**KAMA MNAVYOFAHAMU, LAINI ZA SIMU AMBAZO HAZIJASAJILIWA KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBUSHO CHA TAIFA (NIDA) NA KUTHIBITISHWA KWA ALAMA ZA VIDOLE ZILIANZA KUZIMWA TAREHE 20 JANUARI, 2020 USIKU NA ZOEZI LINAENDELEA.**

**HAKIKI TENA USAJILI WA LAINI ZAKO KWA KUPIGA NAMBA *106# NA UCHUKUE HATUA STAHIKI SASA.**

1.0 KWA WALIOSITISHIWA HUDUMA ZA LAINI ZAO ZA SIMU KUANZIA TAREHE 20.01.2020 WANAWEZA PIA KUENDELEA NA UTARATIBU WA USAJILI KWA LENGO LA AMA KURUDISHA LAINI ZAO ZILIZOFUNGWA KAMA ZITAKUWA BADO ZIPO AU KUPATA LAINI MPYA. ZOEZI HILI NI ENDELEVU.

2.0 KWA WATUMIAJI/WAOMBAJI (WATANZANIA) WAPYA WA LAINI ZA SIMU WATAENDELEA KUSAJILIWA MUDA WOTE KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA TAIFA NA KUHAKIKIWA KWA ALAMA ZA VIDOLE. **HUDUMA HIYO NI ENDELEVU PIA.**

3.0 MATUMIZI SAHIHI YA VITAMBULISHO WAKATI WA USAJILI WA LAINI ZA SIMU (ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE) UKO KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO:-

3.1 Sisi wa-**Tanzania** kitambulisho chetu ni kile cha Taifa kitolewacho na NIDA kwa vigezo vyao;

3.2 Kwa wageni wanaokaa hapa nchini **chini ya miezi sita** wanasajili laini za simu kwa kutumia namba za Hati zao za kusafiria na kuhakiki kwa alama za vidole;

3.3 Kwa wageni wanaokaa zaidi miezi sita wanatumia vitambulisho ***(Legal Resident ID)*** ambavyo hupewa na NIDA (Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa Uhamiaji na NIDA);

3.4 Kwa wanadiplomasia wanatumia Hati zao za kusafiria pamoja na vitambulisho vyao vinavyotolewa na Wizara ya Mambo ya nje; na

3.5 Kwa wakimbizi wanatumia vitambulisho vyao ambavyo hupewa na NIDA (Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa Uhamiaji na NIDA),

4.0 KATIKA KUJIRIDHISHA KUWA WALIOSAJILI LAINI ZAO ZA SIMU WAMETUMIA VITAMBULISHO SAHIHI, TCRA KWA KUSHIRIKIANA NA WATOA HUDUMA ITAFANYA ZOEZI LA KUHAKIKI LAINI ZOTE ZITAKAZOKUWA ZIMESAJILIWA ILI KUWAONDOA WALE WALIOSAJILI LAINI ZAO AMA KWA KUTUMIA VITAMBULISHO VYA WATU WENGINE AU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO TOFAUTI SAMBAMBA NA KUWACHUKULIA HATUA ZA KISHERIA.

5.0 IKUMBUKWE PIA KWAMBA KUSAJILI LAINI YA SIMU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA MTU MWINGINE NI KOSA SANJARI NA KUPEWA LAINI ILIYOSAJILIWA NA MTU MWINGINE.

6.0 ONYO NA TAHADHARI ZINAENDELEA KUTOLEWA KWA MAKUNDI YOTE YALIYOORODHESHWA KWENYE KIPENGELE CHA 3.0 HAPO JUU, KUTOTUMIA KITAMBULISHO KISICHOKUHUSU WAKATI UNASAJILI LAINI ZAKO ZA SIMU (ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE).

**Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**
**24 Januari, 2020**

# KCMC yajitosa upandikizaji mbegu uzazi

**INATOKA UK. 3**

30 hadi 42, wanaume kwa wanawake.

Alitaja sababu za kuwapo kwa tatizo hilo nchini kuwa ni vichocheo vya homoni kutoka kwenye ubongo hadi kwenye mayai na kizazi kutokuwa na uwezo wa kushika mimba.

Alisema pia kuwa na uvimbe kwenye kizazi kwa wanawake, uke kubana kunakotokana na maumbile na kusababisha mwanamke kushindwa kupokea mbegu za kuzalisha mtoto na kuziba kwa mirija ya uzazi kwa wanawake.

Alisema sababu nyingine ni unywaji wa pombe kwa sababu zinaharibu ubora wa mbegu kwa wanaume na wanawake, hivyo wamekuwa wakishauri watu kuacha unywaji wa pombe kupita kiasi.

Dk. Shayo alisema uwiano wa tatizo hilo kwa wanawake unalingana kwa asilimia 40 kwa kila kundi na asilimia 10 kwa kila kundi hakuna sababu za msingi za tatizo hilo.

"Asilimia 40 kwa wanawake na asilimia 40 kwa wanaume wana tatizo hili, ina maana asilimia 80 tatizo hili linasababishwa na mambo niliyoeleza, lakini asilimia 10 kwa wanawake na 10 kwa wanaume hazina sababu yoyote kwa sababu wanapimwa, hawana tatizo, kwa hiyo tunashindwa kujua ni sababu zipi zinawafanya wakose watoto," alisema.

Alisema pamoja na tiba wanazotoa ikiwamo ya vidonge vya kuzalisha mayai ya kusaidia kupata ujauzito, wanatoa ushauri kwa wenza wenye tatizo la kisaikolojia ikiwamo kuwa na mawazo yaliyopitiliza kunakosababisha kutopata watoto.

Alisema pia wanafanya mazungumzo ya kina kuhusu historia ya familia na historia ya tiba alizoanza kutumia mgonjwa ili kufahamu namna ya kumsaidia.

"Pamoja na tiba, tunakaa na mgonjwa au wenza ili kusikiliza historia yao kabla ya kuanza kuwapa kiini cha tatizo na kusaidia kumpa tiba sahihi na kama ikibainika ana tatizo la kisaikolojia, tunawapa ushauri kuwasaidia kupata mtoto," alisema.

# JMP aagiza makinikia kupigwa bei



**INATOKA UK. 2**

Mkuu Barrick) ni picha ya upendo umeeleza ukweli kaka yako alitumwa mwaka 1978 kuja kuipiga Ikulu.

"Leo usingekuwa humu ndani kwa sababu ingekuwa imeshaanguka zamani lakini uvumilivu wa kaka yako wa kuacha kuipiga Ikulu inawezekana hata kaka yako angefia hapa huwezi ukajua. Labda na yeye angepigwa kabla hajapiga lakini ni ukweli kwamba mambo yaliyopita hubaki historia, tuendelee mbele," alisisitiza.

Hatua hiyo, Rais Magufuli alisema sasa wameanza ukurasa mpya ambao ni safi na mambo ya kuongeza bei ili hisa iwe ndogo au kupindishwa kutokana na gharama haitapatikana kwa sababu itakuwa kwa mujibu wa makubaliano.

"Ninaomba pande zote kwa sababu tumekubaliana na Mungu wetu ameona na viongozi wa dini wameshuhudia, mkasimamie makubaliano haya. Wale watakaowekwa kwa upande wa Tanzania kuwakilisha msiende kununuliwa. Mnaweza mkawa mmefanya kazi kubwa kwenye mazungumzo lakini wataokwenda kwenye kampuni badala ya kuangalia maslahi ya nchi wanakwenda kuwasilisha maslahi yao," alisema.

Pia alisema serikali itatoa ushirikiano kwao na vyombo vya ulinzi vitawezesha shughuli kufanyika sawasawa ili pande zote zinufaike.

Pia aliwaeleza walioshiriki mazungumzo hayo kuwa wamefanya kazi na wengine wametoa machozi na kuwaeleza kuwa Mungu atawalipa.

Sambamba na hilo, aliitaka Barrick iitangazie dunia kwamba Tanzania ni nchi bora kwa uwekezaji na wale waliodhani haitawezekana sasa imewezekana. Aliwataka wanapokwenda kutekeleza majukumu yao, wazingatie mazingira na hali za wanaozunguka migodi hiyo kwa kuwajali kwenye huduma za kijamii.

Kuhusu makinikia, Rais Magufuli alisema wakati yakisombwa miaka mingi, Watanzania waliaminishwa ni mchanga.

"Haya mambo yanahitaji uzalendo na kujitoa na bila kujitoa haya yote yasingetokea ninawashukuru sana Barrick. Fikiria kutoka hisa sifuri hadi asilimia 16 na faida itakayopatikana ni ya asilimia 50 kwa 50 huu ni ushindi mkubwa kwa upande wa barrick na Tanzania," alisema.

Naye, Bristow alisema anashukuru mgogoro huo ambao umedumu miaka mitatu umekwisha kwa kukubaliana maeneo tisa.

"Watu wengi waliona msimamo wa Rais Magufuli kama utawafukuza wawekezaji lakini walichofikia ni funzo kubwa kwa sekta ya madini na sehemu zingine," alisema.

Baada ya mgogoro kati ya serikali na Acacia iliyokuwa inasimamia migodi ya Buzwagi, North Mara na Bulanhulu, Rais Magufuli aliunda tume ya kuchunguza mwenendo wa biashara ya madini.

Matokeo ya tume hiyo yalibaini ukiukwaji wa sheria, utaratibu na kanuni zilizopo hivyo kuikosesha serikali mapato inayostahili.

Hatua hiyo ilisababisha serikali kuitoza faini ya Dola za Marekani bilioni 190 jambo lililosababisha kuanza kwa mzungumzo yaliyohusisha pande hizo mbili.

# Wizara Mambo ya Ndani kaa la moto

**INATOKA UK. 2**

10 zilizotajwa na Rais Magufuli.

Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na kushindwa kufuatilia sakata la utekelezaji wa mradi wa ufungaji wa mfumo wa utambuzi wa alama za vidole kwenye vituo vya polisi, maarufu sakata la Lugumi.

Baada ya Dk. Mwigulu kukaa pembeni, Lugola alitolewa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), alikokuwa Naibu Waziri na kukabidhiwa mikoba ya Mbunge huyo wa Iramba Magharibi. Uongozi wa Lugola ulikoma juzi baada ya Rais Magufuli kueleza kuwa maofisa wa wizara hiyo wameingiza serikali kwenye mkataba wa uwekezaji wa vifaa vya zaidi ya Sh. trilioni moja bila kufuata utaratibu uliowekwa kisheria, huku kukiwa na harufu ya ufisadi.

Baadaye jioni, Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilitangaza kuwa George Simbachawene ametuliwa kuchukua nafasi ya Lugola akitokea Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), alikokuwa waziri, hivyo kuifanya idadi ya mawaziri katika Wizara ya Mambo ya Ndani kufikia wanne katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli.

### SABABU ZA CAG

Ingawa hakuhusisha moja kwa moja na baa la kutumbuliwa mara kwa mara kwa mawaziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti yake ya mwaka 2015/16, aliitaja wizara hiyo kuwa miongoni mwa taasisi za serikali zenye madeni makubwa.

Katika ripoti hiyo, CAG alibainisha kuwa wizara hiyo pia ni miongoni mwa taasisi mbili za serikali zinazoongoza kwa kufanya ununuzi mkubwa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, taasisi nyingine inayokula sahani moja na wizara hiyo kwa ununuzi mkubwa nchini ni Shirika la Umeme (Tanesco).

# CCM yashtukia mbinu za kificho upinzani

**INATOKA UK. 3**

washindani wetu.

"Haya nimeyazungumza hadharani, ninajua wanatuangalia kwenye televisheni, wajue mikakati yetu, unapojiamini kuwa ni mchezaji mzuri, unaficha nini namna ya kuchenga, chenga zako?" alihoji.

Aliwataka wana CCM wajizatiti katika hali ya ushindi kwa sababu CCM ya sasa siyo ile ya nyuma na wapinzani wao wa sasa siyo wa nyuma nao wamebadilika na wanabuni mikakati mingi.

"Wana CCM tumejitathmini na kutambua tulikotoka na kujirejesha katika misingi iliyowekwa na wahasisi, madharani kwenye eneo la fedha na uchumi hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo kuhakiki na kurudisha mali za chama na jumuiya zake ambazo zimeongeza mapato toka Sh. bilioni 46.1 mwaka 2015/16 hadi Sh. bilioni 59.8 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 30.

"Baada ya kuthaminisha upya mali za chama katika mikoa 13, thamani yake imeongezeka kutoka Sh. bilioni 41.33 mwaka 2016/17 hadi Sh. bilioni 974.66 hivi sasa, sawa na ongezeko asilimia 2275.3, hii ni kwa mikoa 13 bado mingine tunaendelea," alisema.

Hata hivyo, alisema alipounda Tume ya Bashiru (Katibu Mkuu CCM), yaliyojitokeza ni mengi na ya ajabu ambayo yapo mengine hawakuyazungumza.

Aliwataka kuhakikisha wanahoji miradi inayotekelezwa maeneo yao na kusisitiza kuwa kiongozi yoyote ndani ya serikali akihoji kwa nini anafuatwa, kama hataki aondoke apishe wengine.

"Msikae kimya mkiona miradi ya serikali inadorora waelezeni viongozi wa mkoa na wilaya na mkiona hatua hazichukuliwi, toeni taarifa, mjulisheni Katibu Mkuu wa CCM.

"Tulipobana eneo la ufisadi, tumejikuta tuna fedha nyingi, fedha zilizopo sasa zinaweza kuendesha nchi zaidi ya miezi sita, hata kama tungekuwa hakuna fedha tunakusanya, miezi sita tunaishi." alisema.

Alikumbushia mchakato wa kuwaondoa serikalini watumishi hewa na kueleza kuwa yupo kiongozi aliyekuwa Mamlaka ya Mapato (TRA) ambaye alikuwa na watumishi wake binafsi saba ambao ni hewa na wapo waliokuwa wamesoma na kuishia darasa la pili.

Rais Magufuli alisema ameishi ndani ya CCM na ataondoka akiwa ndani ya chama hicho na atahakikisha yale yaliyoandaliwa, atayasimamia ndiyo maana wakati mwingine amekuwa mkali.

Pia, aliwahakikisha wana CCM kuwa hatawasahau na wasaidizi wake ndani ya serikali wanajitahidi na wengi wameanza kujielewa ndiyo maana mishahara wanapata tarehe 22 hadi 23.

"Fedha zipo, makusanyo ya mwezi yameongezeka, tulipokuja tulikuwa na makusanyo Sh. bilioni 850, mwezi uliopita ilikuwa Sh. trilioni 1.8," alisema.

Pia, alisema wanashirikiana na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, aliyemwelezea kuwa ni mtu mpole, msikivu na hana makuu na kwamba angezaliwa mwingine anayefanana naye, mambo yangekuwa safi.

"Mabadiliko ni makubwa, wapemba na waunguja mnafahamu meli mbili zimenunuliwa, makusanyo kwa mwezi yameongezeka, mishahara imepandishwa, Uwanja wa Amani Abeid Karume unapanuliwa, soko la karafuu halina matatizo sana, barabara zinajengwa, juzi nilikaribishwa shule zinajengwa," alisema.

Awali, Dk. Bashiru alisema maelekezo yote ya Kamati Kuu kushirikisha wadau wote ndani na nje ya chama yanaendelea vizuri na mikoa yote 32 imeshawasilisha kwake mapendekezo yao.

"Uliponielekeza hukunielekeza umewaita kufanya nini au kuzungumza nao nini, hata mimi mwenyewe sijui na pengine na mimi ni miongoni mwa wenye wasiwasi, na kwa sababu sijui ajenda, nakiona kikao hiki kama mkutano mkuu wa joto joto kuelekea kwenye mkutano mkuu wenyewe, kwa idadi na uwakilishi," alisema.







Kamishna wa Polisi Intelijensia ya Makosa ya Jinai, Charles Mkumbo, akizungumza na wananchi wa Kata ya Murieti, wilayani Arusha juzi, katika mkutano maalumu kwa ajili ya kusikiliza maoni pamoja na changamoto, ili kuweka mikakati ya pamoja kukomesha matukio ya kihalifu ya mauaji ya wanawake na ubakaji yanayojitokeza kwenye maeneo yao. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# RC amwagia pikipiki maofisa kata, vijiji

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, ametoa pikipiki sita kwa watendaji sita kati ya wanane katika Kata za mjini Babati, kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la usafiri kwa watumishi wa serikali.

Akizungumza wakati wa kukabidhi pikipiki hizo juzi, Mnyeti alisema kutokana na tatizo la usafiri kwa watumishi wa umma, amegawa pikipiki hizo ili watendaji hao wawafikie wananchi.

Mnyeti alisema pikipiki hizo, zina thamani ya Sh. milioni 14.3 na zimenunuliwa na Halmashauri ya Mji wa Babati, kupitia fedha za kujenga uwezo zitokanazo na uendelezaji wa miji (ULGSP).

Alisema kupatikana kwa vitendea kazi hivyo, ni nyenzo muhimu ya kuwafikia wananchi kupata huduma tofauti na awali kwa kuwa watumishi hao walishindwa kuwafikia wananchi kwa kukosa usafiri wa uhakika.

Kwa mujibu wa Mnyeti, watendaji waliopewa pikipiki hizo ni wale wanaotokea kata za pembezoni mwa mji wa Babati huku akiwasisitiza kutokukaa ofisini badala yake wafike vijijini kutoa huduma kwa wananchi.

"Tunataka tuone kero za wananchi zinatatuliwa. Kama mimi nafika hadi vijijini kwa nini nyie watendaji wa kata na vijiji msifike maeneo hayo. Tumetoa pikipiki hizi, hivyo hatutategemea kupokea kisingizio chochote," alisema Mnyeti. Mkuu wa Mkoa alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Fortunatus Fwema, kusimamia kazi ya kununua pikipiki za maofisa watendaji wa kata za Babati na Bagara.

Fwema alisema wako kwenye mchakato wa kuwanunulia pikipiki watendaji wa kata hizo.

"Baada ya kuwanunulia pikipiki watendaji wa kata zilizo pembezoni tunaahidi kutekeleza agizo lako la kuwanunulia watendaji wawili wa Babati na Bagara ili kukamilisha kata zote nane," alisema Fwema. Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Sadiki Mrisho, alisema pikipiki hizo zinatakiwa kutumiwa kwa matumizi ya kiserikali.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sigino, Evelin Panga, alisema pikipiki hizo zitawasaidia kufika kiurahisi katika shughuli zao vijijini.

Panga ameishukuru serikali kwa kuwapatia nyenzo hizo, ya usafiri kwa kuwa awali walikuwa wanatembea kwa miguu kutoka sehemu moja hadi nyingine.

# Watakiwa kuthamini bidhaa za ndani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WADAU wa mifugo katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, wameitaka jamii, kuachana na dhana potofu ya kudhamini bidhaa zinatoka nje ya nchi kuwa ni bora kuliko zile zinazotengenezwa nchini.

Wakizungumza katika hafla fupi ya kuwakabidhi vyeti iliyofanyika jijini Arusha jana, wadau hao walisema tatizo linalowakabili wawekezaji katika sekta ya mifugo ni uelewa mdogo kwa jamii kuhusu mtumizi ya bidhaa za ndani.

Waliitaka jamii kuwa na utaratibu wa kuthamini na kutumia bidhaa zinazotengenezwa na viwanda vya ndani, ili kuunga mkono juhudi za serikali za kufikia hatua ya uchumi wa kati na wa viwanda

Aidha, waliiomba jamii kuondokana na dhana kuwa bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi ni bora kuliko zinazozalishwa nchini.

Baraka Laizer, mmoja wa wadau hao, alisema wafugaji wengi wameanza kuamka na kufuga kibiashara kwa kutumia malighafi za mifugo, kuanzisha viwanda vikiwamo vya kuchakata ngozi, kufungasha maziwa na nyama kwa kutumia teknolojia ya gesi itokanayo na kinyesi cha ng'ombe.

Laizer alisema tatizo linalowakabili ni ushindani mkubwa wa bidhaa kutoka nje ya nchi, hivyo kuna dhana imejengeka kwenye jamii ya kutokununua bidhaa za ndani, kwa kigezo kuwa bidhaa hizo hazina ubora viwango.

Msimamizi wa Kiwanda cha Uchakataji Nyama cha Maasai Exports Butchery, Frank Mollel, alisema kiwanda chake huzalisha bidhaa za nyama zenye ubora wa kimataifa lakini bado wananchi hawazitumii kwa wingi jambo linalosababisha soko la ndani kusuasua.

"Watu kutoka mataifa ya nje wananunua ng'ombe hapa nchini, wanasafirisha nje ya nchi, na huko wanatumia mashine kama tunazotumia sisi. Lakini wakiingiza bidhaa hizo nchini, Watanzania wananunua kwa wingi na kwa bei ya juu wakidhani ni bora kuliko zetu ilihali kiwango cha ubora kinafanana na bidhaa hizo tunazalisha hapa nchini," alisema Mollel.

Aidha, aliishauri serikali na taasisi zake, kuwa mfano kwa kutumia bidhaa za ndani, ikiwamo nyama zinazozalishwa ndani nchi kwa kufanya, hivyo kutawapa hamasa zaidi wananchi kutumia bidhaa zinazotengenezwa ndani ya nchi.

Leah Sangawe, ambaye ni mfugaji, alisema ng'ombe ni zaidi ya biashara kwa kuwa ana uwezo wa kutoa malighafi nyingi tofauti zinazoweza kuzalisha bidhaa vikiwamo chakula, mavazi, dawa, pamoja na mapambo.

Alitoa rai kwa wafugaji kutokukatishwa tamaa na tatizo ma masoko na kuendelea kuzalisha bidhaaa zenye ubora na ushindani katika soko la kimataifa.

Ofisa Mifugo Halmashauri ya Arusha, Charles Ngiloriti, alisema halmashauri hiyo imejipanga kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili wafugaji, ikiwamo kuwatembelea maeneo yao ya kazi, kuwapatia elimu ili kuongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mifugo.

Naye Daktari wa Mifugo Halmashauri ya Arusha, Dk. Yohana Kiwone, aliwaambia wadau hao kuwa halmashauri ipo kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji wote, hivyo wanatakiwa kutumia fursa hiyo, kutatua matatizo yanayowakabili na kufanya uzalishaji bora unaokidhi viwango vya soko la kimataifa.

## Madiwani Mbulu wamfagilia JPM

**Na Allan Isack,** MBULU

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, limempongeza Rais John Magufuli kwa kufanikisha ujenzi wa miradi ya maendeleo ya hospitali ya Wilaya pamoja na jengo la utawala la makao makuu ya halmashauri hiyo.

Akizungumza katika mutano wa Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa Halmshauri hiyo, Joseph Mandoo, alisema wanampongeza Rais Magufuli kwa kufanikisha ujenzi wa miradi hiyo. Mandoo alisema halmashauri ya Mbulu, imepiga hatua ya kimaendeleo katika sekta za elimu, afya, utawala, miundombinu, kilimo na ufugaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Hudson Kamoga, alisema kutokana na kutengwa kwa fedha hizo, halmashauri hiyo, imezidi kupiga hatua za kimaendeleo kupitia miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa.

"Jengo la utawala la makao makuu linaendelea vizuri na hospitali nayo inaendelea kujengwa katika kata ya Dongobesh, natarajia ujenzi huu utakamilika baada ya miaka mitano," alisema Kamoga.

Alisema wanatarajia kutenga eneo la kumbukumbu ambalo litaandikwa majina ya madiwani waliokuwepo madarakani kipindi cha utekelezaji wa miradi hiyo, wakiongozwa na Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, na Mkurugenzi Mtendaji.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, alisema Rais Magufuli amepeleka maendeleo makubwa kwenye Wilaya hiyo, ikiwamo ujenzi wa miradi ya kimkakati ya muda mfupi ya kipindi cha miaka minne aliyoongoza tangu alipochanguliwa.

"Tumeona barabara za ghorofa, elimu bila malipo, ujenzi wa reli ya kisasa, umeme, ujenzi wa hospitali mpya za Wilaya zimejengwa vituo vya afya, utadhani ameongoza kwa miaka 40," alisema Mofuga.

# Wachangiwa kujenga kituo cha polisi

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

SERIKALI ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, imeanzisha mchakato wa kukusanya fedha kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa Kituo Kikuu kipya cha Polisi cha Wilaya hiyo kitakachojengwa eneo la Dachkona, Kata ya Gararagua.

Uamuzi wa kujenga kituo hicho kipya unatokana na kituo cha zamani kilichoko Kata ya Sanya Juu kukabiliwa na uchakavu wa majengo na miundo mbinu ambayo ilijengwa kabla ya Uhuru.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, akizungumza katika hafla fupi ya kuzindua uchangiaji huo wa hiari juzi, alisema kituo kilichopo ni cha muda mrefu na kilijengwa na wakoloni.

"Ndiyo maana mnaona majengo yake ni chakavu na hayakidhi mahitaji. Tumeona kuna umuhimu mkubwa wa kujenga kituo kipya na cha kisasa kitakachokidhi mahitaji ya askari na watumiaji wengine wa majengo hayo," alisema Buswelu.

Aidha, alisema kituo hicho kipya kinachotarajia kujengwa, iwapo kitakamilika kitaimarisha ulinzi na usalama wilayani humo hasa kwa kuwa wilaya hiyo iko mpakani na nchi ya jirani ya Kenya.

Alisisitiza kuwa: "Haya majengo ni ya zamani sana na wakoloni waliyajenga kwa makusudio yao lakini tukaendelea kuyatumia kama kituo cha Polisi. Kwa sasa tunakwenda kuanza ujenzi wenye miundo mbinu ya kisasa inayoendana na mahitaji ya Polisi."

Ujenzi wa kituo kipya cha Polisi unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 270.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliyekuwa mgeni rasmi, alisema majengo ya kituo cha sasa hayafanani na kazi inayofanywa na Jeshi la Polisi.

Ole Sabaya alichangisha kiasi cha Sh. milioni 5.5 huku baadhi ya wadau, wakiwamo wafanyabiashara, wakiahidi kuchangia Sh. milioni 17.8

Wadau walioguswa na ujenzi huo walitoa ahadi ya kuchangia saruji mifuko 1,302, mtofali 5,860, mawe malori 15, kokoto malori sita na mchanga lori sita hadi kufikia mwishoni mwa mwezi huu.



Mwanaharakati kutoka Kata ya Same, mkoani Kilimanjaro, Zaina Mndeme, akifafanua jambo kuhusu mpango kazi wa namna ya kutokomeza ukatili wa kijinsia unaotekelezwa na Shirika la kiraia la Kwieco wilayani humo, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Sababu kushuka ukeketaji zatajwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI takwimu za matukio ya ukatili wa kijinsia zikionekana kupaa katika Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Diwani wa Arusha Chini, Rodgers Mmari, amesema vitendo hivyo vimepungua baada ya mangariba kutangaza kuacha kazi hiyo.

Mmari alikuwa akizungumza jana wakati wa kikao cha kutathmini matokeo ya mradi wa miaka mitatu wa kupinga ukeketaji katika kata hiyo uliokuwa ukitekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la Tusonge CDO.

Alisema mojawapo ya mafaniko hayo ni baadhi ya wanawake waliokuwa wakijihusisha na shughuli za ukeketaji wa watoto wa kike, maarufu kama mangariba, kuachana na shughuli hiyo mbaya.

"Mangariba hawa si tu waliachana na shughuli za kukeketa watoto wa kike, bali pia wamejiunga katika kupinga mila hiyo potofu huku wakisaidiana na sisi katika kuhakikisha wengine ambao wanaendelea na shughuli hiyo wanaachana nayo", alisema.

Pia katika mchango wake, Mmari alisema mafanikio hayo yametokana na ukweli kwamba uongozi wa shirika la Tusonge uliamua kuwashirikisha viongozi wa kidini, serikali za vijiji na kata, hivyo kuwafikia watu wengi zaidi.

"Kipindi kilichopita elimu kama hii tuliyoipata kupitia Tusonge ilikuwa inawafikia watu wachache kutokana na kazi ya kutoa elimu kufanyika katika ngazi za wilaya na mkoa. Ukweli ni kwamba mradi huu umefika mpaka ngazi ya vijiji na hata vitongoji na nyumba kwa nyumba", alisema.

Mwenyekiti wa Seriakali ya Kijiji cha Mikocheni, ambacho ni moja ya wanufaika wa mradi huo, Evarist Komba, alisema mradi huo umeleta mabadiliko makubwa kutokana na watu wengi kuachana na tabia za kufanya ukatili hasa kwa wanawake na watoto.

"Kabla ya mradi huu, watu walikuwa wakifikiri ya kuwa ukatili waliokuwa wakiwafanyia wake zao au watoto ikiwemo kutekeleza familia zao ulikuwa ni kitu cha kawaida.

Lakini baada ya elimu tuliyoipata hali hiyo imebadilika na kuna furaha katika nyumba nyingi katika eneo letu", alisema Komba.

"Pamoja na kwamba mradi huu ndiyo unahitimishwa, sisi tutaitumia elimu tuliyoipata kwa kuendelea na vita dhidi ya ukatili na tutaifanya kuwa endelevu, kwa kuwa kasi ya maendeleo huwa kubwa pale ambapo hakuna vitendo vya ukatili," aliongeza.

Mmoja wa mangariba walioachana na kazi hiyo, Sarah Koroma, alisema katika kipindi cha likizo za mwisho wa mwaka, wao ndio hutumia fursa hiyo kuwakeketa watoto wa kike.

Alisema Desemba kila mwaka, kwa mfano, alikuwa na uwezo wa kukeketa watoto kati ya 30 na 40.

"Niwahakikishie wananchi ya kuwa nimeachana na kazi hii rasmi na sasa nimeungana na viongozi wa serikali pamoja na taasisi ya Tusonge katika kuwashawishi wenzangu ambao wanaendelea na ukatili huo kuachana nayo", alisema Koroma.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Tusonge, Agnatha Rutazaa, aliwapongeza viongozi na wananchi wa Kata ya Arusha Chini kwa ushirikiano waliotoa kwa shirika hilo katika kipindi chote cha miaka mitatu cha utekelezaji wa mradi huo.

"Ushirikiano tuliupata kutoka kwa wananchi, viongozi, viongozi wa Kidini, walimu pamoja na wanafunzi ulipelekea mafanikio ya mradi huu na pia serikali kuweza kutambua juhudi ambazo tumekuwa tukizifanya katika vita dhidi ya ukatili kwa wanawake na watoto," alisema.

## Rais wa wasanii atoa ya moyoni

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

RAIS wa Mtandao wa Wasanii wa Injili Tanzania (Tagoane), Dk. Godwin Maimu, ameeleza kufurahishwa kwake na mkakati wa serikali wa kumaliza tatizo la makazi ya askari Polisi na Kituo Kikuu cha Polisi Wilaya ya Siha.

Maimu alieleza hisia zake jana, baada ya serikali wilayani humo kuzindua harambee ya uchangiaji wa ujenzi wa kituo hicho.

"Ndugu zangu wana Siha wenzangu, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mkuu wetu wa Wilaya pamoja na Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa kazi nzuri wanazozifanya ila kwa upekee kuleta wazo la kujenga jengo jipya la kituo cha Polisi. Ni jambo zuri kwa sababu badala ya kukarabati majengo yaliyojengwa zamani tangu enzi za ukoloni tunajenga jipya," alisema Maimu.

Alitaka kila mkazi wa Siha na wale waishio nje ya Mkoa wa Kilimanjaro, kwa namna moja au nyingine kuchangia ujenzi huo, kwa kuwa atanufaika kwa ulinzi wa raia na mali zake.

"Kidogo ulicho nacho kina thamani kubwa katika ujenzi huo. Pia niwatie moyo kuwa tuwashirikishe hata marafiki zetu wenye uwezo wa kuchangia wafanye hivyo.

"Kwa kujali umuhimu wa kuwa na kituo hicho chenye hadhi ya wilaya yetu, nimechangia kiasi cha pesa kidogo Sh. milioni tatu ikiwa ni pamoja na kugharimia gari la matangazo na vyombo, mafuta na vijana kufanya matangazo Siha na viunga vyake kwa siku mbili, maandalizi ya harambee, saruji mifuko 20 na tofali 300."

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, kituo cha zamani kilichopo Sanya Juu, kwa sasa kinakabiliwa na uchakavu wa majengo na miundombinu ambayo ilijengwa kabla ya Uhuru.



## HABARI DODOMA



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Basungwa, akizungumza kwenye semina iliyoandaliwa na Wakala wa Vipimo (WMA), kwa wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Seleman Sadiq na Katibu wa Kamati, Zainab Mkamba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WMA yatakiwa kukagua vituo vya mafuta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, imeshauri Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA), kuweka mkazo zaidi katika vituo vya mafuta kutokana na baadhi kufanya udanganyifu wa vipimo hususan siku za Jumamosi na Jumapili.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Suleiman Saddiq, baada ya kuhitimishwa kwa semina kwa wabunge wa kamati hiyo iliyotolewa na wakala huo, jijini hapa.

Alisema kuna tatizo kwenye vituo vya mafuta kutokana na baadhi kufanya udanganyifu vipimo na kuwaibia wateja siku za mwisho wa wiki.

"Unakuta mtu wa vipimo aliendа Alhamisi au Ijumaa pampu ziko sawa. Lakini akienda Jumamosi anakuta pampu ile ile inatoa mafuta kiwango tofauti na mwanzo," alisema.

Aliomba eneo hilo liwekewe mkazo ili wanaofanya vitendo hivyo wachukuliwe hatua bila kuoneana aibu na vituo vinavyorudia makosa hayo vipewe adhabu kali zaidi ili Watanzania wasiendelee kuibiwa.

Aidha, alisema wakala huo ni mdau mkubwa katika Tanzania ya viwanda na vipimo ndivyo vinawapa haki katika ununuzi wa aina mbalimbali.

"Tunaomba waendelee na jitihada wanazofanya. Wametueleza matatizo yao na sisi kama kamati tumechukua tutapeleka ndani ya bunge ili kuishauri serikali kama vile suala la rasilimali watu,"alisema.

Naye Mbunge wa Igalula, Mussa Ntimizi, alisema wakala huo una wajibu wa kumlinda mlaji na kushauri serikali iangalie namna ya kudhibiti na kutoa adhabu kali sana kwa wale wanaowaibia kwa kuwapunja wanapofanya ununuzi.

Kwa upande wake, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema ushauri walioutoa wabunge, wizara imechukua ili kufanya maboresho na wakala utatue kero zinazowakabili Watanzania.

Alisisitiza WMA kutoa elimu na kuagiza taasisi zote zinazotoa huduma kwa Watanzania kutoa elimu kwa kina ili kuondoa kero kwa wananchi.

Kuhusu magunia kutokuwa na uzito sawa, Waziri Bashungwa alisema serikali inaliangalia kwa karibu ili kusiwe na kero hiyo kwa wakulima.

Awali Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Dk. Ludovick Manege, alisema semina hiyo ililenga kuwaelimisha wabunge wa kamati hiyo kuhusu majukumu ya wakala na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne.

"Jukumu letu ni kumlinda mlaji katika vipimo vinavyofanyika, na matumizi ya vipimo viwe sahihi, ili mnunuaji wa bidhaa apate stahiki ya kipimo sahihi na serikali kupata mapato sahihi," alisema.

Alisema Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pia inategemea kupata takwimu sahihi kutoka kwa wakala huo ili kuona tozo zinazotolewa zinaendana na vipimo sahihi.

"Tuna changamoto ambazo tunaziona kwetu ni fursa, kwa mfano mabadiliko ya teknolojia, uchache wa watumishi, Wakala lazima ijipange kupima bidhaa zote viwandani ili zinapoingia sokoni ziwe kwenye vipimo sahihi," alisema.

Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hicho kuwa ni kukamilisha kwa kituo kikubwa cha kupima malori ya mafuta kilichoko Kibaha.

"Tulikuwa na kituo chetu Ilala ambacho kilikuwa kinapima magari mawili hadi matatu, lakini kwa sasa kilichopo kinapima magari 70 kwa siku," alisema.

Kadhalika, alisema wamefanikiwa kufanya uhakiki kwenye madini kwa kuhakikisha mizani yote inayotumika ni sahihi ili serikali ipate mapato sahihi bila udanganyifu.

# Vijana wapewa mtonyo kugombea uongozi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIJANA nchini wametakiwa kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu, badala ya kuwa vibaraka wa wanasiasa. Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Dodoma Mjini, Saidi Kasote, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuwahamasisha vijana kuchangamkia kugombea ubunge na udiwani kwenye uchaguzi huo.

Alisema badala ya kusubiri kutumiwa na wanasiasa wakati wa uchaguzi, ni wakati wao sasa kuchangamkia fursa hiyo muhimu kwa kuwa wako miongoni mwao wenye sifa za kuwa viongozi.

"Ninawaomba mwaka huu 2020 kwenye uchaguzi mkuu, vijana wa Dodoma mjini msikubali kutumiwa na wanasiasa hawa watakaojitokeza badala yake na ninyi mjitokeze tena kwa wingi kuwania nafasi hizo," alisema. Alisema Rais John Magufuli amewaamini vijana na amewapa nafasi mbalimbali za uongozi, hakuna sababu ya kuwa vibaraka. Pia aliwataka watakapopewa nafasi hizo na wananchi kufanya kazi kwa bidii ili taifa lipate maendeleo zaidi.

# Tahadhari homa ya mafua makali

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema hadi sasa Tanzania haina mgonjwa wa mafua makali yanayosababishwa na kirusi kipya aina ya Corona, huku ikitoa tahadhari mbalimbali kwa wananchi ili kuepuka kupata ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa wizara hiyo, Gerald Chami, mafua hayo yamezikumba China, Thailand, Japan, Korea Kusini na Marekani kuanzia mwanzoni mwa Desemba, mwaka jana.

"Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa huo tangu ulipotokea, na unaambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa majimaji yenye virusi," ilisema taarifa hiyo.


Alisema takwimu za mlipuko huo zinaonyesha kuwa hadi Januari 22, mwaka huu, watu 560 wameathirika huku vifo vikiwa 17.

"China imethibitisha wagonjwa 550 na vifo 17. Nchi nyingine ni Thailand wagonjwa wanne bila kifo, Hong Kong wagonjwa wawili bila kifo, Marekani, Taiwan na Japan zimethibitisha kuwa na mgonjwa mmoja bila kifo," iliongeza taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mpaka sasa Tanzania haina mgonjwa wala mshukiwa wa ugonjwa huo na kutoa tahadhari kwa wananchi kutokana na kuwapo na mwingiliano mkubwa wa kibiashara na nchi hizo hususan China.

Dalili za ugonjwa huo ni homa na mafua makali, kuumwa na kichwa, mwili kuchoka, kikohozi, kubanwa mbavu, maumivu ya misuli, vidonda vya koo, kuathiri mapafu na kupumua kwa shida.

Kutokana na tishio hilo, wananchi wametakiwa kutokuwa na hofu ya ugonjwa huo kwa sababu wizara inaendelea kuchukua tahadhari ili ugonjwa huo usiingie nchini.






Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja (kushoto), akizungumza baada ya kupokea gari la kubebea wagonjwa katika halmashauri hiyo, juzi. Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Majengo ya mahakama kukarabatiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, amesema serikali itaendelea kuyafanyia ukarabati mkubwa majengo ya mahakama mjini na vijijini ili kuwawezesha wananchi kusikiliza mashauri yao kwa nafasi nzuri.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Kamati ya Katiba Sheria na Utawala Bora ya Baraza la Wawakilishi iliyokutana na uongozi wa Wizara hiyo ofisini kwake Mazizini, mjini hapa.

Waziri alisema ukarabati wa majengo hayo unaendelea Unguja na Pemba na kwamba upande wa Pemba, Mahakama ya Chake Chake imefanyiwa matengenezo makubwa na kurudisha hadhi na haiba yake.

Aidha alisema jengo la Mahakama Kuu limefanyiwa ukarabati mkubwa kwa kuongeza baadhi ya nafasi za vyumba vya majaji na mahakimu.

"Kazi ya kuyafanyia majengo ya Mahakama Unguja na Pemba inaendelea. Tumefanya ukarabati huo katika mahakama za vijijini, Makunduchi hadi Mfenesini," alisema.

Pia alisema serikali inakusudia kujenga jengo la kisasa la Mahakama Kuu huko Tunguu Wilaya ya Kati Unguja ili kuwawezesha wananchi kupata nafasi ya kusikiliza mashauri yao mbalimbali.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala Bora, Dhulfa Mmaka, alisema ujenzi wa jengo jipya la Mahakama kuu la Tunguu litapunguza msongamano uliokuwa katika Mahakama ya Vuga kwa wananchi katika kusikiliza mashauri yao.

"Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la kisasa la Mahakama Kuu ambalo litakuwa na nafasi kubwa zaidi kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati mmoja," alisema.

Mhandisi wa Ukarabati huo, Mussa Ali, alisema kazi ya ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Tunguu unaendelea ingawa umekumbwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa mchanga.

"Ujenzi unaendelea kwa sababu tunataka kukamilisha na kukabidhi baadhi ya hatua za ujenzi mwaka huu ingawa zipo changamoto za uhaba wa mchanga ambao ndiyo tegemeo katika utekelezaji wa mradi huu," alisema.

Baadhi ya maofisa wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, wamesema kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kisasa la Mahakama Kuu kutatoa nafasi kubwa kwa watendaji ikiwamo majaji, mahakimu na maofisa wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

"Kukamilika kwa mradi wa jengo la makao makuu ya Mahakama huko Tunguu utatoa nafasi nzuri kwa wananchi kuja na kusikiliza kesi zao kwa nafasi pamoja na watendaji nao kuwajibika kwa kupanga siku za kusikiliza mashauri muafaka," alisema Mrajis wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Mohamed Ali Mohamed Shein.

# SMZ kuanzisha kozi usanifu majengo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema inakusudia kuanzisha fani ya usanifu wa majengo ili kuwa na wataalamu wa kutosha katika eneo hilo.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alisema hayo jana alipozungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo kikuu cha Ardhi huko Forodhani, Unguja.

Alisema vyuo vikuu vya Zanzibar havina shahada ya usanifu wa majengo, hivyo kuwafanya wanafunzi wanaosomea taaluma hiyo kwenda nje ya Zanzibar.

Simai alisema malengo ya Zanzibar ni kuwa na wataalamu wake ambao watatumika kwa ajili ya kazi za ujenzi zinazofanywa na serikali katika wizara na taasisi zake mbalimbali.

"Tunataka kuwa na vyuo ambavyo vitatoa wahitimu waliobobea katika masomo ya usanifu wa majengo ambao ni wazalendo," alisema.

Naibu Waziri alisema ziko kasoro mbalimbali zimejitokeza katika usimamizi wa miradi na majengo ya serikali ambayo yapo yaliyojengwa chini ya kiwango huku akibainisha kuwa serikali imeingia katika hasara kubwa katika baadhi ya miradi ya ujenzi ambayo ni ya kiwango cha chini.

Naye mwakilishi wa wanafunzi wa msafara huo, Fatuma Mohamed, aliitaka serikali kutoa kipaumbele cha kwanza kwa wahandishi wazalendo kuona wanapewa miradi ya ujenzi muhimu kwa kuzingatia viwango.

Alisema iko mifano ya baadhi ya miradi ya ujenzi ambayo imepewa wazalendo na kuonesha uwezo mkubwa wa kuzingatia viwango vya ubora na usanifu wake.

"Wahandisi wazalendo kilio chao ni kutaka miradi ya ujenzi inayotekelezwa na serikali kuona wanapewa ili kuendeleza taaluma hiyo," alisema.

# Aonya ukataji ovyo mikoko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Ali Suleiman, amewataka wananchi kuacha kukata miti aina ya mikoko kwa matumizi ya kuni ili kulinda uhifadhi wa mazingira.

Akizungumza juzi wakati kamati hiyo ilipofika eneo la Kisakasaka kuangalia uharibifu wa mazingira, alisema licha ya kuwapo kwa juhudi za kuotesha mikoko kwa wingi katika maeneo yaliyoathirika kimazingira, wako baadhi ya watu wamekuwa wakikata mikoko hiyo.

Suleiman alisema Zanzibar kuna zaidi ya maeneo 50 ambayo yameathirika na uharibifu wa mazingira huku baadhi yake maji ya bahari yakiingia katika makazi ya wananchi.

"Zanzibar inakabiliwa na athari kubwa za kimazingira na njia pekee ni kuotesha Mikoko katika fukwe kwa ajili ya kuzuwia matukio ya uharibifu wa mazingira," alisema.

Suleiman akifuatana na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi walitembelea maeneo ya Kisakasaka kuangalia shughuli zinazochukuliwa na kuotesha mikoko.

"Tumesikitishwa na matukio ya ukataji wa mikoko licha ya juhudi za kuotesha kwa ajili ya kudhibiti kasi ya maji kuvamia maeneo hayo," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mazingira, Sheha Mjaja, alisema ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira kukata mikoko iliyooteshwa kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

Alisema Zanzibar inakabiliwa na athari ya uharibifu wa mazingira zaidi ikiwamo maeneo ya fukwe na njia pekee ni kuotesha Mikoko kwa ajili ya kuzuia kasi ya maji kupanda juu na kuingia katika makazi ya wananchi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, baadhi ya maeneo katika kisiwa cha Pemba yako salama baada ya wananchi kuchukua juhudi za kuotesha mikoko kuzuia kasi ya maji ya bahari.

"Mamlaka ya Hifadhi ya Mazingira agizo letu kubwa wananchi waoteshe mikoko kwa wingi ili kuzuia kasi ya maji ya bahari kuvamia makazi ya wananchi," alisema.

Zaidi ya asasi za kiraia na vikundi vya ushirika 60 vimeshiriki katika kupanda mikoko katika mwaka huu kwa ajili ya kulinda hifadhi ya mazingira.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JANUARI 25, 2020



**BURNA BOY HAUWEZEKANI TENA**

Soma UK.20



## MWENDO WA KUACHWA

# Kaanza Stamina, sasa Mabeste analia

BASI SAWA

## Dully Sukes ajivunia kuitwa Mkongwe

MSANII mkongwe katika muziki wa kizazi kipya, Dully Sykes, amesema hakuna ubaya kuitwa jina hilo kwa sababu bado anaenda sawa na vijana.

Akizungumza na EATV & EA Radio Digital, Dully Sykes alisema jina la mkongwe ni sawa heshima na yeye hawezi kujifananisha na vijana.

"Wasanii wengine ukiwaita wakongwe wanakataa kwa sababu wameshindwa kuendelea kufanya vizuri, kwahiyo ukimuita hivyo anaona unazidi kumkandamiza, mimi kila siku nafanya vizuri, nikiitwa hivyo nachukulia sawa tu" amesema Dully Sykes.



## Baba wa Diamond azidi kumwachia Mungu

BABA wa mwanamuziki wa Bongo fleva, Diamond Platnumz, Mzee Abdul, amezidi kumlilia mtoto wake akisema utajiri aliokuwa nao si jambo la busara kumuacha yeye baba yake akihangaika kwa umaskini.

Akizungumza na mtandao wa Dar24, Mzee Abdul ameeleza jambo hilo linamuumiza hasa akiangalia anamvyomtuza mama yake Bi Sandra katika maisha ya kifahari, huku akimuacha yeye akiendelea kusota katika maisha duni.

"Mtoto wake tajiri anauwezo lakini hakufanyii hivi, wengi wanataka wanione mimi natembelea gari nakaa kwenye nyumba nzuri, wanione nina vitu vizuri vizuri tuu, na kitu ni chake katafuta yeye ndio mwenye uamuzi anaweza kusema leo baba nimfanyie hivi, ila mimi hata sasa hivi akisema asinifanyie chochote kwangu ni sawa tu, siwezi kuanza kupiga kelele kwa sababu katafuta mwenyewe" amesema Mzee Abdul.





## Wolper kula bata kwa sana tu

MWIGIZAJI nyota wa Bongo muvi, Jacqueline Wolper, amewataka watu kutohoji maisha yake ya gharama kwa sababu yeye ana uwezo na kujua njia ya kupata fedha.

Akiongea na EATV, Wolper, amesema kuwa bora pesa zake azitumie kula bata, kuliko ikatokea siku amedondoka halafu watu wakaanza kugombania pesa zake ambazo hawakuzitafuta.

"Siwezi kupunguza kula kwa sababu natafuta sana pesa, halafu mimi sitaki kuua watu kwa ajili ya pesa zangu kwa mfano nadondoka mtu anakuja kugombania pesa zangu ambazo nimezitafuta mwenyewe," amesema.

## INSTA-TWITTER





**Go Champ** Mpira pasi ndiyo siri ya ushindi. Samagoal sasa ile mipande ya Grealish kama naizoom hivi unavyoitia nyavuni. Go Champ-**Roma Mkatoliki.**



**Umeendelea** kutupa sababu zaidi ya bilioni Watanzania tuendelee kupenda EPL. Naamini wafuatiliaji wa EPL wa Tanzania watakuwa wameongezeka. Funga wote, Liver Jogoo, bomoa daraja. All The Best Aston Villa-**Madee Ali.**



# Mmmh! Lavalava hapoelekea takuwa kweli

IMAYE mwanamuziki wa bongo fleva, Lavalava, onesha muongozo wa uhusiano wake na malkia wa mu nchini, Irene Uwoya, ambao unaonekana kuwa ou kuingia katika mahaba mazito.

kiongea hivi karibuni, Lavalava amesema kuwa yeye rene Uwoya ukaribu wao hauna maana nyingine uti na ushkaji, lakini mrembo huyo anamvutia kama anamume.

woya ni mwanamke ambaye anamvutia mwana- he yeyote yule lakini mimi na yeye ni washkaji tu una kingine, nashangaa hizi stori sijui zimeanzia i"

valava alipoulizwa ni msanii gani wa kike anaem- a kimapenzi amesema anavutiwa na Uwoya na ni anamke ambaye anatamani kua nae kimahusiano Mimi namwangalia sana Uwoya ni mwanamke ekamilika kila idara ana tabia nzuri sana anafaa 'Wife Material' akipika chai utafikiri kapika biriani" sema.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...

# Mbosso amkumbuka Marther kihisia

MWANAMUZIKI kutoka lebo ya WCB, Mbosso, ameamua kutoa hisia zake za maumivu kwa mama mtoto wake, Marther, ambaye alifariki mwaka mmoja uliopita.

Kupitia akaunti yake ya SnapChat, mwanamuziki huyo aliweka picha ya marehemu mpenzi wake na kuandika ujumbe ambao umeashiria simanzi yake ya hali ya juu. Kaandika maneno katika lugha ya kiingereza yenye maana "Lini nitakuona tena" na kuweka 'Emoji' yenye ishara ya maumivu.

Marehemu Martha alifariki hapo mwaka jana, wawili hao walidaiwa kuzaa mtoto, licha ya kuficha mahusiano yao.



# DJ Khaled atangaza ujio wa mtoto mwingine

RAPA wa Marekani, DJ Khaled, ametangaza ujio wa mtoto wake wa pili na mkewe Nicole Tuck.

Tangazo hilo ameliweka katika akaunti yake ya Instagram ikiambatana na picha yake na mkewe wakiwa wanafurahia.

Bila kutaja jinsi ya mtoto wao huyo, amesema mama na kichanga hicho wanaendelea vizuri na kuomba marafiki zake na mashabiki kuwaombea.



## INSTA-TWITTER

Tuffollow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Tufanye** kazi kwa juhudi. Bahati huja baada ya juhudi zetu. Hongera sana Bro Samagoal-**Dulla Makabila.**



**Najisikia** furaha sana kukuona ulipo Samagoal. Mwenyezi Mungu akutangulie. Tuko nyuma yako kwa dua nzuri-**Ali Kiba.**



**Kimsingi,** kubwa baada ya hii sina deni na EPL kwenye maisha yangu ya ushabiki wa mpira. Ahsante Captain Diego Samagoal. Haina Kufeli haswaa-**Mwana FA.**

## Kuumbe!



MWENDO WA KUACHWA

# Kaanza Stamina, sasa Mabeste analia

SASA imekuwa kama mtindo mpya kwa wasanii wa muziki wa Bongo Fleva, kuanika nje siri zao za ndani kwa sababu tu, kuachwa na wake zao.

Alianza rapa anayeunda kundi la Rostam, Stamina, ambaye licha ya kulalamika kuachwa na mkewe, aliamua kutunga wimbo kwa ajili ya kulalamika huku akimtuhumu mchezaji mmoja wa timu ya Simba kwamba amesababisha tatizo hilo.

Kutoka kwa wimbo huo 'Asiwaze' kuliibua mjadala mkali kutoka kwa mashabiki ambao kuna wale waliopinga hatua hiyo wakidai ni udhalilishaji kwa sababu kuachana ni jambo la kawaida katika ndoa.

Kuna waliomuunga mkono wakisema ni haki yake kutoa kile alichokuwa nacho moyoni na kinamuumiza, hivyo kuelezea maumivu yake kuhusu aliyekuwa mke wake ni kama anasafisha nyongo.

Wakati mjadala huo haujapoteza nguvu, msanii mwingine Mabeste amekuja na yake, yeye kibaya zaidi anadai ndoa yake imevunjika kwa sababu mke wake Lisa alikuwa akimsaliti kwa kuwa yeye ni maskini.

Akizungumza na EATV & EA Radio Digital, Mabeste amesema kuwa mzazi mwenziye ndiyo aliomba talaka jambo ambalo limemuumiza sana.

"Mimi na yeye tulikata hizo stori tangu mwaka jana, tulikuwa hatuongei na hata watoto hajawahi kuniletea niwaone nikimtumia ujumbe kuhusu familia yangu hanijibu, alinifata akaniambia tuachane nikakubali," amesema Mabeste.

Hata hivyo, kinachomuuma zaidi ni kitendo cha aliyekuwa mke wake kwenda kuishi na rafiki yake ambaye wanafanya kazi pamoja.

"Kinachoniumiza mtu ambaye ameenda kuishi naye ni rafiki yangu ambaye tunafanya kazi" amesema Mabeste.

Aidha Mabeste ameendelea kumwaga siri "Siwezi kumtaja huyo rafiki yangu anayeishi naye kwa sasa, ila ni muongozaji wa video 'Director'. Nilikuwa namuuliza kitu gani kinaendelea anakataa, mke wangu nilimpa uhuru sana, kumbe alikuwa akitoka Moshi kuja Dar analala kwa jamaa, mimi ananidanganya kwamba yupo kwa dada yake" ameongeza.

Hata hivyo akazidi kusema kwamba baada ya kumpa talaka aligundua mwanamke huyo alimkataa kwa sababu hakuwa na pesa za kutosha kama anavyotaka.



# Warembo mastaa 'waliomwish' Samatta



AMBER RUTTY

NANDY

**Na Adam Fungamwango**

HABARI ya nchi, Nahodha wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Mbwana Samatta, kujiunga na klabu ya Aston Villa inayoshiriki Ligi Kuu nchini England, imepokelewa kwa shangwe na Watanzania.

Samatta amelamba mkataba mnono wa miaka minne na nusu akitokea Genk ya Ubelgiji.

Waliposikia habari hizo tu, Wabongo wakavamia kwenye akaunti ya instagram ya Aston Villa, wengine wakipongeza na wengine wakionyeshwa kushangazwa na ucheleweshwaji huo.

Mara tu baada ya kutangazwa, mtandao huo ulivamiwa na mashabiki wengi kutoka Tanzania na lugha ya Kiswahili ndiyo ikawa inatawala, unaweza ukadhani ni instagram ya klabu moja pale Manzese.

Hata baadhi ya wazungu walionyeshwa kushangazwa na wingi wa Wabongo kuingia kwenye mtandao wa kijamii wa Aston Villa, wengine wakishangazwa na lugha iliyokuwa ikitumika, kwani hawaifahamu.

Taarifa zinasema kuwa wakati wa tetesi za Samatta kuhamia timu hiyo zilipoanza, mtandao wa instagram wa klabu hiyo ulianza kuongeza idadi ya watu walioingia, ambao inadaiwa wengi wao walikuwa ni Wabongo.

Viongozi wa Serikali, vyama vya siasa, watu maarufu, wanamuziki na wasanii mbalimbali wamekuwa wakituma salamu za pongezi wa Samatta kwa kuwa Mtanzania wa kwanza kucheza Ligi Kuu ya England.

Mbali na mastaa hao, wapo mastaa wa kike ambao nao kwenye akaunti zao za kijamii, walijaza na kupamba picha za staa huyo na 'kumuwishi'

**AMBER RUTTY**

Ni mmoja wa wasanii wa kike nchini na mpamba video. Yeye ni mmoja kati ya wasanii wa kike waliopamba picha za Samatta kwenye mtandao wake wa instagram na akaandika maneno mafupi tu kuonyesha kufurahishwa na mchezaji huyo mkazi wa Mbagala kufanikiwa kupenya na kucheza Ligi Kuu ya England 'Hongera Sana'. Ni maneno aliyoyaandika Amber Rutty.

**NANDY**

Mmoja kati ya wasanii wachache wa kike ambao wako kwenye chati ya hali ya juu kwa sasa.

Yeye naye hakuna nyuma, bali ameweka picha za Samatta kwenye mtandao wake wa instagram na kuandika maneno yafuatayo 'Viva Samatta, hongera'.

**SHILOLE**

Mwigizaji na mwimbaji, Shilole naye hakuna nyuma kumpongeza Mbwana Samatta. Na yeye kwa furaha yake alitupia picha ya mchezaji huyo akishika jezi ya timu yake mpya ya Aston Villa na kutengeneza kichwa chake cha habari kifupi tu 'Samatta Champion'.

**PAULA KAJALA MASANJA**

Huyu ni binti wa mwigizaji nguli nchini, Kajala Masanja. Binti huyu anajiita Paula Kajala Masanja.

Naye hakuna nyuma kwani kwenye mtandao wake wa kijamii, aliweka picha ya Mbwana Samatta na kuandika maneno matamu ya kumpongeza 'Tanzania tunajivunia wewe. Mungu akusimamie naye kila hatua."

IMETOKEA

# Mama atamani kujiua kwa kuzidiwa na ndevu

THERESIA Mumbi (34) ni mama wa mtoto wa kiume mwenye miaka saba, kazi yake ni utingo wa magari ya daladala katika mji mkuu wa Nairobi nchini Kenya.

Lakini maisha yake huwezi kusema ni ya kawaida kama ya mwanamke mwingine, kutokana na kuwa na ndevu nyingi kama mwanaume.

"Nilipokuwa shuleni nilikuwa na nywele nyingi, kwangu mimi niliona kwamba ni jambo la kawaida, hivyo hazikunisumbua sana " Mumbi anasema

Alipomaliza shule ya sekondari na kuanza kutafuta ajira, Mwaka 2005 aligundua kwamba nywele zake zilikuwa zinakua kwa kasi, hivyo aliamua kuanza kuzinyoa, lakini kumbe ndio aliharibu na kuzifanya ziongezeke zaidi.

Theresia anasema kuwa aliogopa sana maisha yake yatakuwaje?

"Niliona kuwa ni kazi ngumu ya kuficha hali hii ya kunyoa ndevu kila wakati, kwani nilikuwa nazinyoa kila saa, na nikaanza kuchoka nikaamua kuwa sitazinyoa tena" alisimulia Mumbi.

Wakati alipokuwa na desturi ya kunyoa hakuwa na changamoto zozote kwani alifanana kama wanawake wengine wa kawaida.

Pale alipoacha kunyoa, masaibu mapya yalianza kumpata, kwani alikuwa ana muonekano mwingine, alianza kuandamwa na watu kwa kumwangalia kwa kumshangaa na kumnyooshea kidole, huku wakimpa majina mengi ya kejeli.

Wakati huo alikuwa anafanya kazi kama mhudumu katika hoteli moja, hapo ilikuwa rahisi kwake kwani wale wateja walimzoea muonekano wake , ila matatizo aliyapata wakati akitoka nje ya eneo lake la kazi.

"Nikiwa nyumbani nilikuwa sitoki nje kabisa, hata kama ningekuwa na njaa vipi, nilikuwa nasubiri hadi giza liingie ilimradi niende dukani au sokoni kununua mboga au chakula,"Mumbi aliongezea kusema

"Nilikuwa naona aibu ili jirani zangu wasinione na ndevu alafu waanze kuzua gumzo mtaani, ingawa sikuwa na shida na sehemu yangu ya ajira"

Haya yote yalichangiwa na kukua kwa ndevu zake pamoja na kuharibika kwa ngozi yake.

Mumbi aliamua kutafuta msaada wa daktari na huko aliambiwa kuwa mwili wake ulikuwa na hitilafu ya homoni iliyosababisha yeye kuwa na nywele hizo.

Kisa kimoja ambacho Mumbi hatawahi kukisahau ni wakati alipokamatwa na polisi akiwa kazini.

Siku hiyo anasema kuwa ilikuwa tofauti kwani anadai kuwa maofisa waliwataka kila mtu atoe shilingi mia nne za Kenya au apelekwe rumande, Mumbi anasema kuwa hakuwa na hela hizo .

Kwa hiyo yeye na baadhi ya wahudumu wa magari ya matatu(daladala) waliwasilishwa katika kituo cha polisi , walipofika huko yeye aliwekwa katika sehemu ya wanawake , baada ya muda ofisa mmoja wa kike aliingia kwenye gereza aliyokuwa Mumbi na kumuamrisha atoe nguo zake.

Alipomuuliza kwa nini? alimjibu

"Hatuna uhakika kuhusu jinsia yako na tunahofia kuwa wewe ni mwanaume , kwa hivyo tunataka kukukagua ili tuthibitishe "

Mumbi anasema tukio hilo lilimhuzunisha sana kwani polisi hao walimdhalilisha kwa kuwa alikuwa na ndevu.

Mumbi anasema kuwa kitendo kile kilimfanya ajiulize maswali mengi na pia kumuuliza Mwenyezi Mungu kwanini alimuumba akiwa hivyo ?

Haikuwa rahisi kwake kujikubali kwani wakati mmoja alitaka kujitoa uhai wake, lakini alijifariji kutokana na mtoto wake kukubali tatizo lake.






Chaupele

# Mwisho wa ubaya aibu

Na Adam Fungamwango

DUNIANI kuna mambo ya ajabu sana. Unakuta binadamu anafurahia kutesa binadamu mwenzake. Baba anamtesa mtoto wa kambo, au mama anamnyanyasa mtoto wa kambo. Kisa tu hakumzaa yeye. Lakini hakumbuki kuwa ni mtoto wa mkewe au mumewe wa sasa.

Kwenye jamii yetu ya Kiafrika ni mambo ambayo yamezoeleka na kuna hadithi nyingi juu ya hili. Miaka nenda rudi, tumesikia hadithi hizi huko nyuma, lakini eti hadi leo karne ya 21 ambapo tayari watu wameshakuwa na upeo mkubwa, wengine wakiwa na elimu za juu, lakini bado mambo haya yapo.

Ndiyo maana hata watunzi wa filamu bado wameendelea kulisisitizia ili kutoa elimu kwa jamii kuepukana na tabia hii.

Filamu ya 'Chaupele' inatukumbusha kuwa bado mambo hayo yapo kwenye jamii, lakini pia inafundisha kuwa siku zote unapomfanyia ubaya mtu, hata kama hukuchukuliwa hatua za kisheria, lakini Mwenyezi Mungu anaweza kukuadhibu kwa mkono wake na kukuacha na aibu.

Imechezwa na baadhi ya wasanii ambao ni mastaa nchini kama Grace Mapunda, Zuberi Mohamed maarufu kama Niva, mzee Muhogo Mchungu na wengineo. Muhogo Mchungu anafiwa na mkewe. Anaachiwa binti wa miaka 16, aitwaye Mwanaidi. Kutokana na upweke, Muhogo Mchungu anaoa mke mwingine kwa ajili ya kumtunza yeye na binti yake pia.

Mke huyo ambaye ni Grace, anaolewa na Muhogo Mchungu akiwa tayari ana mabinti wengine wawili ambao ni Amina na Shani.

Kama walidhani kuwa nyumba ingekuwa na furaha tena, walikosea. Kilichokuja kwenye nyumba hiyo ni mateso, manyanyaso na maafa.

Muhogo Mchungu anasafiri kwenda mjini kwa shughuli za kibiashara. Kwa bahati mbaya anapata ajali mbaya wakati anarejea na kufariki dunia.

Mkewe mpya ndiye anarithi nyumba hiyo. Hakuna mwanamke mzuri, kwani baada ya hapo alimgeuza Mwanaidi kuwa hausigeli badala ya binti yake. Mama huyo na mabinti zake wawili walimnyanyasa na kumbagua binti huyo, na pamoja na kufanya kazi zote



za nyumbani hapo, lakini alibadilishiwa malazi akawa analala na mifugo.

Kila kukicha mateso yalizidi, leo ni afadhali ya jana. Jina likabadilika kutoka Mwanaidi na kuwa Chaupele kutokana na kuwa na ukurutu mwili mzima.

Mtoto wa mtemi wa kijiji hicho alikuwa amerejea kutoka mjini kwa masomo. Mtemi alitaka sasa awe na mke. Niva ambaye ndiye mtoto wa mtemi, awali alikataa baada ya kuona kama vile hakuna msichana mrembo kijijini hapo anaweza kumfanya ampende.

Baba yake akaamua kuandaa ngoma ili wasichana wote wa himaya yake waje kucheza kwa ajili ya kumpa fursa kuchangua mchumba.

Wasichana wote walijipamba na kwenda kwa mtemi ili kujaribu bahati, wakiwemo watoto wawili wa Grace, Amina na Shani ambao waliokuwa wakipewa nafasi kubwa.

Ni Mwanaidi tu ndiye aliyebaki nyumbani. Alitokewa na mzimu wa mama yake na kumuuliza kama anataka kwenda ngomani. Akakubali. Aligeuza kuwa msichana mzuri, akiyevaa nguo za gharama.

Akaenda ngomani. Mtoto wa mtemi alipomuona, hakutaka kupoteza muda. Chaupele akawa ndiye mke wa mtoto wa mfalme na kuwaacha mabinti wa mama yake wa kambo, wakilia na kulaumiana.

WAMEACHANA

# Wendy, Kevin waliishi miaka 22 kwa mashaka





SASA ni rasmi kwamba ndoa ya Wendy Williams na Mume wake Kevin Hunter imefika mwisho.

Wendy Williams ambaye ni mtangazaji wa shoo za TV na mwigizaji na Kevin Hunter, wameachana kisheria baada ya talaka kutolewa hivi karibuni.

Kulingana na mtandao wa TMZ, mwisho wa ndoa hiyo ilikuwa siku ya Jumanne ya wiki hii, baada ya jaji wa mahakama moja ya New Jersey, kuidhinisha talaka hiyo.

Nyaraka za talaka hiyo inaeleza namna ya wawili hao . wanavyoweza kugawana baadhi ya mali ambazo walizipata wakati wa ndoa yao.

Watalaka hao wanatakiwa kugawana sawa mali hizo ikiwamo nyumba wanazomiliki.

Katika mgawanyo huo, Wendy anachukua nyumba iliyopo Florida ambayo anaishi mama yake kwa sasa, huku Kevin anakamilisha mpango wa kuchukua nyumba nyingine iliyopo Morristown, New Jersey.

Hata hivyo haijafahamika kama katika mgawanyo huo utahusisha kampuni ya utayarishaji wa vipindi ambayo wote wanamiliki idadi sawa za hisa. Imeelezwa Kevin Hunter anataka kuuza hisa zake kwa Wendy na hivyo kujipatia fedha nyingi.

Wendy atahusika na fenicha zote za ndani, wakati huo huo Kevin atapata haki ya kuchukua magari ya kifahari aina ya Ferrari na Rolls-Royce. Taarifa ya kuachana kwanza iliibuka katika mitandao ya kijamii mwaka jana, baana ya Kevin kuonekana akiwa karibu na mwanamke mwingine Sharina Hudson.

Kulingana na mtandao wa PageSix, nyota huyo wa vipindi vya mazungumzo alikuwa akihangaika kuokoa ndoa yake na Kelvin, lakini jitihada zake hazikufanikiwa.

Fununu za Kelvin kuwana uhusiano wa kimapenzi na Sharina, zilizidi kumchanganya Wendy na hasa taarifa ya mwanamke huyo kutarajia kupata mtoto.

Kelvin na Sharina imeelezwa walikuwa na uhusiano huo katika kipindi cha miaka 10, jambo ambalo liliumuathiri Wendy na kuamua kuomba talaka ili kujiweka sawa kiakili.

Pia imeelezwa nyaraka za talaka hiyo imehifadhiwa katika ulinzi mkali, ili itakapotokea tatizo lolote iwe rahisi kuchukuliwa hatua.

Wendy Williams na Kelvin wamedumu katika ndoa hiyo kwa miaka 22, lakini muda wote waliishi kwa mashaka.



# Burna Boy hauwezekani tena

MIAKA michache ya mafanikio, mwanamuziki wa Nigeria, Burna Boy, ameamua kuweka wazi mali zake ikiwamo jumba la kifahari, magari na mamilioni ya pesa yakiwa benki.

Burna Boy, ameposti video fupi ikimonyesha akiwa ndani ya mjengo wake huo wa kifahari pamoja na msururu wa magari ya bei mbaya anayomiliki.

Nyumba hiyo anayomiliki ambayo inaitwa condo ipo katika eneo la Beverly Hills nchini Marekani.



## Uche hatakagi kumung'unya maneno

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Uche Maduagwu, amesema baadhi ya wasanii wa filamu wanachuki na Mercy Johnson, kutokana na kutambulisha kazi mpya.

Kulingana na Uche, baadhi ya wasanii wameshindwa kuhudhuria uzinduzi wa filamu mpya ya Mercy, kutokana na wivu na roho mbaya.

Msanii huyo aliweka tuhuma hiyo katika mitandao ya kijamii akisema waigizaji wakubwa hawawezi kuonesha tabia hiyo ya kuunga mkono kazi za wengine kutumia Instagram.

## Empress mshukuru Mungu wako

MKALI wa Nollywood ambaye amepata mashabiki wengi, Empress Njamah, amenusurika kifo baada ya yeye na mama yake kushambuliwa na wezi.

Empress aliweka jambo hilo katika akaunti yake ya Instagram na kusema anamshukuru Mungu kwa kumnusuru kutokana na tukio hilo la kutisha.

Amesema tukio kama hilo linawafanya watu waliopitia jaribu ya kifo kuwa karibu na Mungu kila wakati.





## John Legend awasha moto Nigeria

MKALI wa muziki wa taratibu ambaye anapenda kuvaa suti nyeupe, John Legend, amekuwa miongoni mwa wasanii wa Marekani waliotumbuiza nchini Nigeria.

Legend alikuwa mjini Lagos siku ya Jumatatu ilipanda jukwaani na kuimba nyimbo zake bora ambazo zilionekana kuwapagawisha mashabiki wake.

Mshindi huyo wa Grammy alikuwa mwanamuziki aliyealikwa katika sherehe ya utoaji tuzo za Thisday zilizofanyika katika hoteli ya Eko Hotel Convention Centre iliyopo katika kisiwa cha Victoria.

## Vico ni kweli au unataka kiki?

MWIMBAJI chipukizi, Vico amemshtaki rapa Zlatan, akidai amempiga wakati akiwasaidia marafiki wake wasishambuliwe.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram na kuposti video ikimuonesha akiwa na majeraha usoni na kumtuhumu mwanamuziki Zlatan kuwa ndiye aliyempiga huko Lekki, Lagos.

Katika video hiyo, Vico amesema wanaume ambao idadi wanafikia wanane walimkamata na kuanza kumpiga na kumsababishia majeraha. Anayemkumbuka ni rapa huyo ambaye alikuwapo katika tukio hilo.





**MIONZI YA SHERIA**

Na John Juma
0716217615

# Unafanyaje kushtakiwa mara ya pili kwa kosa lile lile?

MAREJEO ya hilo ni katika makosa ya madai yaliyo katika mashauri ya madai. Japo jambo hilo lipo hata katika makosa ya jinai yu mkini makala hayatajielekeza huko.

Basi yafaa ifahamike kuwa, mtu aliyeshitakiwa kwa kosa fulani, kesi ikasikilizwa na hukumu ikatolewa akashinda au akashindwa, ni kuwa kesi ya namna hiyo, haitakiwi kufunguliwa tena. Isifunguliwe tena mahakama hiyo hiyo au nyingineyo nchini.

Haiwezekani kesi iliyosikilizwa na kutolewa uamuzi kufunguliwa tena. Yapo yanayoweza kufuata baada ya kesi kwisha, kwa mfano rufani, marejeo na mapitio, lakini sio kufungua tena upya.

**YANAYOZINGATIWA**

Yapo mambo ya kuzingatia, ili kesi iliyokwisha isifunguliwe tena. Kwanza, ni lazima wahusika wawe walewale. Haiwezekani Mtu 'A' alimfungulia kesi 'B' na ikasikilizwa na kutolewa uamuzi, halafu 'A' huyohuyo akamfungulia

tena ' B' kesi ile ile kwa kosa lile lile.

'A' anaweza kumfungulia 'B' kesi nyingine, ikiwani kwa kosa tofauti na lile la awali lililokwisha kuamuliwa utaona kinachozuiwa ni mtu yuleyule na kwa kosa lilelile.

**KWA NINI HILO?**

Iwapo hili litatokea wenye wajibu wa kulizuia ni watu wawili. Kwanza ni wajibu wa mshitakiwa kuieleza mahakama kuwa kesi hii ilishahukumiwa sehemu fulani na hapa imerudiwa. Ni wajibu wa mshitakiwa au mwakilishi wake awe wakili au vinginevyo.

Pili, ni wajibu kwa jaji au hakimu anayesikiliza kesi hiyo, kufanya utafiti kupitia kumbukumbu za mahakama na kuliona hilo ili kulizuia.

Hata hivyo, wajibu mkubwa ni mshitakiwa kwa kuwa jaji au hakimu, wakati mwingine anaweza asiligundue hilo hasa ikiwa kesi hiyo iliisha mahakama nyingine na sasa imefunguliwa upya mahakama nyingine. Hivyo, tunaweza kusisitiza kuwa wajibu mkubwa upo kwa mshitakiwa mwenyewe kwa sababu yuko katika nafasi nzuri ya kujua historia ya kesi yake kuliko mwingine awaye.

**ADHABU MAHAKAMANI**

Ikiwa mshitakiwa ataielekeza mahakama kuwa kesi iliyo mbele yake iliwahi kuamuliwa pahala fulani au mahakama yenyewe, ikaligundua hilo basi adhabu kubwa ikayotolewa ni kulitupilia mbali shauri hilo. Kulitupilia mbali ni kulifuta kabisa.

Na juu ya hilo, mahakama kama itapendezwa inaweza kutoa amri ya kulipa gharama. Mshitaki atatakiwa kumlipa mshitakiwa gharama alizotumia, mpaka hapo kesi ilipoishia.

**SHERIA INAKATAZA**

Kifungu cha Tisa cha sheria ya mwenendo wa mashauri ya madai ndicho kinachokataza jambo hili. Kitaalamu, jambo hilo limeitwa Res Judicata.

Kifungu kinasema kuwa hakuna mahakama itakayosikiliza na kuamua shauri kama hilo hilo, linalohusu watu wale wale na madai yaleyale,na ambalo lilishasikilizwa na kuamuliwa na mahakama nyingine yenye mamlaka.

Lengo kuu la kuzuia jambo hili ni kuwa hakuwezi kuwa na hukumu mbili zinazohusu suala moja. Hukumu ni moja, kwa shauri moja nchi zima .

# Wazazi wanavyojibu uhaba wa madarasa

**Na Sabato Kasika**

MUHULA wa masomo kwa shule za msingi na sekondari umeanza Januari 6 mwaka huu.

Wanafunzi wanaendelea masomo yao, licha ya kuwapo na upungufu wa madarasa unaotokana na dadi kubwa ya watoto waliofaulu kidato cha kwanza na wale walioanza elimu ya msingi.

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wazazi, wameanza kuchukua hatua kwa kujenga madarasa mapya kwa ajili ya kutatua tatizo hilo.

Kutokana na upungufu huo imesababisha wanafunzi kuwarundikane katika chumba kimoja cha darasa au kusoma kwa zamu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amewaagiza wakuu wa mikoa kusimamia ujenzi huo na kuhakikisha unakamilika haraaka.

Agizo hilo limepokelewa vyema na baadhi ya wazazi ambao wameamua kujitolea kutumia nguvukazi yao kukamilisha madarasa. Miongoni mwa wazazi hao ni wale wanaoishi kata za Bulinga, Nyamrandirira, Bugwema wilayani Musoma, Mkoa wa Mara.

Kata ya Nyamrandirira, ambayo idadi ya wanafunzi waliofaulu ni 202, imegeuza vyumba vitatu vya maabara katika sekondari kongwe ya Kasoma, kuwa madarasa ya muda. Kulingana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Vincent Anney, wazazi wameamua kushiriki katika ujenzi wa madarasa manne katika kijiji cha Seka, ili wanafunzi hao wahamie huko.

"Wamejiwekea muda kwamba kufikia Machi 30 mwaka huu, madarasa hayo yawe yamekamilika, na mimi nitasaidia upatikanaji wa mchanga na mawe, mbunge



Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, akizungumza na wakazi wa Kata ya Nyamrandirira alipokwenda kuhamasisha ujenzi wa madarasa.



Mafundi wakipanga mbao kwa ajili ya kuweka renta kwenye moja ya madarasa ya Shule ya Sekondari Bulinga.**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

pia ameahidi kutoa mifuko 100 ya saruji," anasema Dk. Anney.

Mkuu huyo wa Wilaya anasema wakazi wa kata ya Bugwema, wamekubaliana kukamilisha ujenzi wa madarasa manne na ofisi mbili za walimu kwa ajili ya Sekondari ya Bugwema.

Anafafanua kuwa katika kata hiyo wanafunzi 249 waliochaguliwa, 114 pekee wameripoti shuleni kutokana na kukosa madarasa.

"Hii ni taarifa ya mkuu wa shule ambayo ameitoa kwenye kikao mkutano ambao tumekubaliana ujenzi wa madarasa ifanyike haraka," anasema.

Anasema, wanafunzi hao 114 wanasomea chumba kimoja, na kwamba hali hiyo imesababisha uelewa kuwa hafifu.

"Niseme kwamba kila mzazi ambaye mtoto wake bado hajaripoti shule ampeleke haraka, vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa," anasema. Dk. Anney anaitaja pia Sekondari ya Bulinga kuwa imepokea wanafunzi 157 wa kidato cha kwanza, wakati inakabiliwa na uhaba wa madarasa matatu.

Hata hivyo, wazazi wameanza ujenzi wa madarasa hayo.

"Wananchi wamejitolea kuchangia nguvukazi na kutoa kiasi cha shilingi 11,000 kila kaya ili kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo, hii itatuaondolea kero ya upungufu wa madarasa," anasema.

**TATIZO LA UTORO**

Kiongozi huyo anasema mtindo wa baadhi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoripoti shuleni kwa wakati umeota mizizi, kwa hiyo ni lazima kuudhibiti.

Katika ripoti ya mkoa huo inaonesha katika halmashauri ya Wilaya ya Musoma Musoma, watoto 3,480 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, 684 pekee wameripoti shuleni.

Kwa upande wa Manispaa ya Musoma, waliofaulu ni 3,748, lakini 951 tu ndio waliosajiliwa shuleni. "Serikali haiwezi kuvumilia hali hiyo, kwa kuzingatia kwamba wazazi wamepunguziwa mzigo wa kusomesha, na sasa elimu inatolewa bure, hivyo wazazi wanatakiwa kuhakikisha kila mtoto anapelekwa shule," anasema.

Mkuu huyo wa wilaya anawaagiza wazazi wa kuhakikisha wanawapeleka watoto wao shule haraka hata kana hawana sare za shule. "Lakini cha kushangaza ni wanafunzi walioripoti shuleni kuwa chini ya asilimia 20, kwa mfano Shule ya Sekondari ya Mugango, ambapo ni wanafunzi 37 tu wameripoti, kati ya 320 waliochaguliwa," anasema.

Aidha, anasema vyumba vya madarasa madarasa 36 vimejengwa, katika wilaya hiyo ambapo yatakamilika kabla ya Februari 15.

# NZIGE TISHIO JIPYA

## ■Kenya, Somalia, Ethiopia hakutamaniki
## ■Wanaruka km 150, wanafikia milioni 40

**Mwandishi wetu**

NCHI za Kenya, Somalia na Ethiopia, zinakabiliwa na tishio la uhaba wa chakula baada ya juhudi za kukabiliana na Nzige kushindikana.

Tayari Umoja wa Mataifa umetoa wito kwa mataifa mengine kuingilia kati kwa kusaidia kukabiliana na nzige hao ambao wamevamia maeneo ya Afrika mashariki.

Hata hivyo nchi jirani zinazopakana na nchi hizo zimetahadharishwa kuwa macho kwani kuna tishio wadudu hao waharibufu wanaweza kuenea hadi kufika Uganda.

Msemaji wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa mataifa (FAO), amesema athari mbaya inaweza kutokea ikiwamo baa la njaa, utapiamlo na kuathirika kwa mfumo wa maisha ya kila siku.

Ethiopia, Kenya na Somalia zinapitia wakati mgumu kukabiliana na makundi ya nzige ambako hakujawahi kutokea kwa miaka mingi. Shirika hilo katika taarifa yake inasema kwamba idadi ya nzige hao huenda ikaongezeka mara 500 zaidi ifikapo Juni mwaka huu.

Ethiopia na Somalia hazijawahi kushuhudia nzige wa aina hiyo kwa kipindi cha miaka 25 huku Kenya ikiwa ni mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 70.

Sudani Kusini na Uganda pia zipo katika hatari ya kuingiliwa na nzige hao ambao wanaendelea kuongezeka na kusambaa.

"Kasi ya kusambaa kwa nzige hao na kiwango ambacho wanavamia maeneo siyo kawaida kiasi cha kuwa changamoto hata kwa mamlaka za kikanda na kitaifa," inazungumza FAO.

Hata hivyo, hatua pekee inayoweza kuwadhibiti ni matumizi ya ndege ambazo zinanyunyiza dawa ya kuua wadudu.



Nzige hao wamesambaa kuanzia Yemen hadi maeneo mengine ya Bahari ya Shamu.

Uchunguzi umebaini kiwango kikubwa cha mvua mwishoni mwa 2019, kilitengeneza mazingira mazuri ya kuzaliana wadudu hao.

Tatizo kama hilo pia limeikumba nchi za India, Iran na Pakistan, ambako huenda wakaanza kusambaa kwa makundi ifikapo msimu wa chipukizi.

Nzige wanaweza kusafiri umbali wa kilomita 150 sawa na maili 93 kwa siku, na kila mmoja mkubwa anaweza kula kiasi kikubwa cha chakula kwa siku.

Novemba mwaka jana, Umoja wa mataifa ilionya kwamba huenda nzige wakavamia baadhi ya maeneo ya Ethiopia na kusema kuwa huenda wakasambaa hadi Ethiopia na Kenya iwapo hawatakabiliwa.

Baadhi ya wakulima nchini Ethiopia wa eneo la Amhara walipoteza mazao yao yote.

Mwezi ulipita kundi la nzige lilazimisha ndege ya abiria nchini Ethiopia, kubadili safari yake.

Wadudu hao waliingia kwenye injini, kioo na sehemu ya mbele ya ndege, na kulazimika kutua katika uwanja wa ndege wa Addis Ababa.

**WASIWASI WATANDA**

Wakazi wanaoishi katika maeneo yaliyovamiwa, wameelezea wasiwasi wao huku viongozi na wataalamu wakiahidi kuweka mikakati ya kukabiliana nao.

Baadhi ya wakazi wa Kaskazini mwa Kenya wamelalamikia uvamizi wa Nzige ambao athari yake inaendelea kuongezeka kwa kuathiri mimea.

Mbunge wa Eldas, Aden Keynan, anasema hiyo inaonesha jinsi gani wanavyotishiwa uhai wao na wadudu hao. Kwa mujibu wa Idara ya Kilimo ya Kaunti ya Wajir, siku ya kwanza Nzige hao walivamia zaidi ya kilomita 30 ya kilimo, akisema baadhi ya wakazi walijaribu kuwafukuza kwa kupiga kelele, kugonga vyuma na honi za magari ili kuwashtua, lakini ilishindikana.

Mtaalamu wa masuala ya mazingira, anaelezea kwamba mabadiliko ya hali ya anga yamechangia pakubwa uvamizi wa nzige hao.

Kulingana na FAO, Nzige hao wanaruka kilomita 150 kila siku, ambapo kundi la Nzige milioni 40 kwa siku wanaweza kuharibu mazao yanayoweza kuwalisha watu 35,000, Ngamia 20 na Ndovu sita.

Kundi moja pekee la Nzige hao wameharibu chakula kinachoweza kuwalisha takriban watu 2,500 kwa mwaka.

**KWA MSAADA WA MTANDAO**



Baadhi ya wananchi wa Kenya wakipambana na nzige.

MAKALA

# Mwaka mmoja wa Rais Felix Tshesekedi madarakani

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Felix Tshisekedi, ametimiza mwaka mmoja tangu kukalia nafasi hiyo ya juu katika taifa la Jamhuri ya kidemokrasi ya Congo.

Kuingia kwake madarakani kumezua malalamiko kutoka kambi ya upinzani, lakini wengi walipongeza wakisema ni hatua ya kihistoria kupatikana kwa nguvu ya kura.

Viongozi wote waliomtangulia walikalia kiti hicho baada ya kumwaga damu kwa kufanya mapinduzi.

Kama mgombea mkuu wa chama cha upinzani cha UDPS, Tshisekedi alimshinda Martin Fayulu, mgombea aliyekuwa akipigiwa upatu na mtangulizi wake, Joseph Kabila, katika uchaguzi huo wa mwezi Disemba 2018.

Alipokalia kiti hicho, alikabiliwa na changamoto nyingi ukiwamo kukithiri kwa ufisadi, miundo mbinu mibovu, vita Mashariki mwa nchi hiyo na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola.



Rais Felix Tsheseked, akisimikwa kushika wadhifa huo na mtangulizi wake Josephn Kabila mwaka jana.

**MZOZO WA MASHARIKI**

Wakati alipotawazwa kuwa rais, aliahidi kujenga Congo yenye udhabiti kwa lengo la kuvutia maendeleo kupitia amani na usalama.

Tshisekedi amejaribu kuimarisha usalama kwa kutoa muda waasi kujisalimisha na wale waliokaidi waliamrisha jeshi kufanya opersheni kuwaondoa msutuni.

Pamoja na juhudi hizo, wananchi wana hofu kutokana na kusuasua kwa operesheni hiyo pamoja na idadi kubwa ya raia wanaouawa na waasi.

Jeshi limefanikiwa kulirudisha nyuma kundi la wapiganaji wa ADF, kundi la waasi ambalo linatoka Uganda lakini sasa limepiga kambi katika jimbo la Beni nchini humo.

"Wakati wa kampeni zangu za uchaguzi , nilipata fursa ya kutembelea ,maeneo haya na nilikumbwa na tatizo hili ambalo linaniumiza moyo sana" , Tshisekedi ameambia BBC.

"Nilichukua jukumu wakati huo la kufanya kila kitu ili kuleta amani".

Rais huyo aliliamuru jeshi kuweka kambi yake mjini Beni ambao umeshamiri mashambulizi ya ADF. Baadhi ya wanajeshi walibadilishwa, na kuleta nguvu mpya katika vita dhidi ya wanamgambo hao.

Katika vita vyake dhidi ya kundi jingine, viongozi wawili muhimu wa waasi wa Kihutu nchini Rwanda (FDLR) waliuawa.

Makundi mengine madogo ya wanamgambo bado yanaendeleza kuwa tishio katika jimbo hilo huku wengine wakihusishwa na biashara haramu ya madini.

Mashambulizi dhidi ya raia yanaendelea huku makundi ya waasi ambayo hujihami na mapanga yakitekeleza mashambulizi wakati wowote.

**MLIPUKO WA EBOLA**

Wakati alipochukua madaraka , Tshesekedi alikabiliwa na tatizo la kuenea kwa virusi vya ebola , mashariki mwa taifa hilo.

Umekuwa mlipuko mbaya wa Ebola duniani , ambao shirika la afya duniani WHO liliutangazza kama janga la kiafya linalohitaji dharura.

Kulingana na Shirika hilo, watu 3,416 waliathiriwa na ugonjwa huo, 2,237 walikufa na wengine 1,136 walinusurika.

Kutoaminiana kati ya wenyeji na maofisa wa afya , kunakosababishwa na mila, ukosefu wa habari, pamoja na mashambulizi dhidi ya maofisa wanaokabiliana na ugonjwa huo kulizorotesha kazi ya kupambana na Ebola.

Serikali ya Tshisekedi ikiwa imepata usaidizi kutoka kwa mashirika ya kigeni na inaonekana kwamba kiwango cha maambukizi kimepungua, lakini WHO inasema ni vigumu kuthibitisha hilo kwa kuwa kuna maeneo kadhaa hayajafikiwa.

**SURUA YALETA UATATA MPYA**

Rais Tshisekedi pia amelazimika kukabiliana na ugonjwa wa Surua. Virusi hivyo vimesambaa kwa kasi na kuambukiza zaidi ya watu 300,000 tangu kulipuka kwa ugonjwa huo mwaka 2019.

Taarifa inasema ugonjwa huo umeenea katika mikoa 26 ya taifa hilo.

Takriban watu 6,000 wamefariki, idadi ambayo inazidi ya wale wa Ebola, kulingana na WHO na kufanya ndio mlipuko mbaya zaidi kuwahi kutokea kote duniani.

Serikali ya Tshisekedi, WHO na mashirika mengine ya kimataifa imewapatia chanjo zaidi ya watoto milioni 18 walio chini ya umri wa miaka mitano nchini humo.

Lakini ukosefu wa fedha za kununua chanjo za kutosha na barabara mbaya umezuia uwezo wa wahudumu wa afya kumfikia kila mtu.

**KUKABILIANA NA NJAA**

Kutokana na mapato ya mtu wa kawaida, DR Congo ni mojawapo ya mataifa yalio na umasikini mkubwa zaidi duniani licha ya kuwa na utajiri wa madini.

Raia wengi wa Congo huishi chini ya dola mbili kwa siku. kulingana na takwimu ya benki kuu ya dunia, lakini taifa hilo lina hatua kubwa za kupiga.

Rais anasema kwamba anataka kukabiliana na umasikini na katika juhudi hizo ameongeza matumizi ya serikali.

Katika kipindi cha miezi 12, bajeti ya serikali iliongezeka kutoka dola biloni sita, hadi kufikia 11.

Ulipaji kodi katika maeneo mengine , ikiwamo katika majengo, umeongezeka ili kulipia matumizi. Lakini watu wengi wa wanasubiri kuona iwapo hali yao ya kiuchumi itaimarika.

**WASIWASI WA KISIASA**

Licha ya kushinda urais, Tshisekedi amelazimika kukabiliana na nguvu ya mtangulizi wake Joseph Kabila, ambaye anamiliki idadi kubwa ya wabunge bungeni.


Majadiliano kati ya vyama hivyo viwili yalichukua takriban miezi saba, kabla ya makubaliano kuafikiwa kwa lengo la kuunda serikali.

Uhusiano kati ya vyama hivyo ulisababisha wasiwasi mkubwa katika kipindi cha mwaka mmoja huku wanasiasa wa pande zote mbili wakilumbana mara kwa mara na wakati mwingine kupigana.

Lakini inaonekana kuna juhudi za kuhakikisha kwamba mambo yanafanyika.

Wafungwa wa kisiasa wameachiliwa huru, huku wapinzani wa kisiasa waliokuwa wakiishi nje ya nchi hiyo wamesamehewa na kurudi nyumbani.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 29 00)



Dondoo: Kulia
1. Mji mkuu wa Mali
7. Lipia bidhaa
8. Hekima
9. Nyumba ya ibada
12. Shetani
14. Shauku ya jambo
15. Ardhi inayozalisha mazao
16. Heshima
18. Hutoa nuru usiku angani
21.Ng'amua
22. Chimbuko
23.Kata nywele
26. Wingi wa neno ini
27. Andaa kitanda ili ulale
28. Mji mkuu wa Vietnam

Dondoo: Chini
1. Kuwa na wasiwasi
2. dohani
3. safisha mwili
4. Mfuasi wa chama cha siasa
5. Utajiri alio nao mtu
6. Ukosefu wa nywele kichwani
9. Huzungukwa na maji
10.Ziwa Victoria nchini Kenya
11. Tarakimu
13. Beirut ni mji wake mkuu
17. Kitu atoacho mkopaji
19. Dalili ya jambo
20.Hutumika kuingilia ndani
24.Kitu anachotaga ndege
25. Karo ya shule

### Jibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| T | A | B | A | K | A | | A | | A | | A | |
| H | | U | | | G | E | R | E | Z | A | N | I |
| A | N | G | O | L | A | | I | | U | | D | |
| M | | I | | | | S | A | M | A | D | I | |
| I | M | A | R | I | K | A | | A | | E | K | A |
| N | | | E | | | M | A | D | I | B | A | |
| I | L | E | J | E | | A | | E | | E | | |
| | E | | E | | M | K | O | B | A | | K | |
| A | M | O | S | I | | I | | E | L | E | W | A |
| | A | | H | | | | | | M | | A | |
| | Z | | A | N | Z | A | | M | A | O | N | I |
| | | | | J | | S | | | S | | Z | |
| Z | A | M | B | E | Z | I | | M | I | R | A | A |



Raia wa China akiwa amejikinga dhidi ya virusi vya Corona kwa kutumia kitambaa cha puani

# VIRUSI VYA CORONA

## ■Vyayumbisha dunia kupata tiba, kinga
## ■Kujikinga kwa 'maski' kwa waibua utata

**Na Mwandishi wetu**

MATAIFA ya Afrika mashariki yametangaza kuchukua hatua ya tahadhari kukabiliana na virusi vya Corona vinavyosababisha maradhi ya homa kali ya mapafu.

Mtu akipata virusi hivyo anakuwa na homa kali ambayo anashidwa kupumua na wakati mwingine husababisha kifo.

Mpaka sasa idadi ya watu waliofariki kutokana na mlipuko wa virusi hivyo nchini China imeongezeka na kufikia 26.

Afrika Mshariki ikiwamo Tanzania ni mshirika mkuu wa kibiashara na China, maelfu ya raia wa nchi hiyo wanaingia kila siku kufanya kazi mbalimbali ikiwamo kutalii.

Kenya, Uganda na Tanzania zimeanza kuchukua hatua kwa kutoa tahadhari na kufanya uchunguzi abiria wanaowasili katika mataifa hayo..

Maofisa wa China wanasema mpaka juzi kuna visa vipya 830 vya maambukizi ya virusi hivyo vimethibitishwa.

Wataalamu kutoka shirika la Afya Duniani wamesema ni mapema kutangaza mlipuko wa virusi vya Corona kuwa janga la kimataifa.

Kufikia sasa karibu miji 10 katika mkoa wa kati nchini China ambayo ina watu milioni 60 imewekewa vikwazo vya usafiri ili kukabiliana na kusambaa kwa virusi hivyo.

Mataifa mengine yalioathiriwa na virusi hivyo ni Vietnam na Singapore, Thailand, Japan, Taiwan, Korea Kusini na Marekani.

**IPI NJIA SAHIHI KUJILINDA?**

Uvaaji wa kitambaa puani inaelezwa ndio njia sahihi ya kukabiliana na virusi hivyo, na katika nchi zilizothibitisha kukumbwa na tatizo hilo wanashauri watu wake kuvaa pale wanapotoka ndani.

Kitambaa hicho cha kuziba mdomo ambacho ni maarufu katika nchi nyingi duniani kwa ajili ya kujizuia maambukizi, kinatumika sana China huku watu wakipewa ushauri wa kuejiepusha na mahali palipo na msongamano wa watu.

Wataalamu wa afya wameelezea namna kutumia kifaa hicho ili kuzuia virusi.

Kitambaa cha puani kilianza kutumika kwa mara ya kwanza katika hospitali mwishoni mwa karne ya 18, lakini zilikuwa hazitumiki katika sehemu za umma mpaka mlipuko wa mafua ulipotokea Uhispania.

Dkt David Carrington, kutoka chuo kikuu cha St George, mjini London, Uingereza, aliiambia BBC kuwa 'Maski' zinazotumika wakati wa operesheni au upasuaji huwa haziwezi kufanya kazi vizuri katika maeneo ya umma.

Anasema kitambaa cha aina hiyo hakiwezi kufanya kazi vizuri dhidi ya virusi vya bakteria wa hewa ambao wanaambukiza, kwa sababu zina nafasi za wazi na zinaacha macho wazi.

Lakini zinaweza kupunguza maambukizi kwa kiasi fulani ya kuwakinga watu katika maambukizi ya mkono na mdomo.

Utafiti uliofanywa kutoka New south Wales, ulipendekeza kuwa watu huwa wanashika nyuso zao mara 23 kwa saa.

Profesa Jonathan Ball, kutoka chuo kikuu cha Nottingham, anasema kuwa katika utafiti mmoja uliofanywa hospitalini, unaonesha 'maski' ya sura huwa nzuri kwa kuzuia maambukizi kama ilivyobuniwa.

Wabunifu waliotengeneza kifaa hicho kwa namna ambayo inaweza kuzuia vimelea vya hewani.

Ingawa ukiangalia ufanisi wake kwa ujumla katika msongamano wa watu, takwimu zinaonyesha utofauti mdogo.

"Vilevile si rahisi kwa mtu kukaa na kifaa hicho kwa muda mrefu ," Prof Ball aliongeza.

Dkt Connor Bamford, wa taasisi ya afya ya Wellcome-Wolfson, iliyopo chuo kikuu cha Queen Belfast, anaeleza kuwa kuweka mazingira safi ni hatua rahisi na nzuri kwa kinga.

"Utekelezaji wa kuweka mazingira safi ndio hatua rahisi zaidi ambayo inaweza kufanya kazi kwa uhakika". anasema

Hata hivyo, China yathibitisha kwamba virusi vya Corona vinaweza kusambazwa kwa njia ya hewa.

"Kuziba mdomo wakati unapiga chafya, kunawa mikono, na kujizuia kuziba midomo kwa mikono kabla ya kunawa, kunaweza kupunguza hatari ya maambukizi kupata virusi", anasema.

Dkt Jake Dunning, mkuu wa masuala ya afya nchini Uingereza anatilia shaka kifaa hicho akisema "Ingawa kuna watu wanahisi kuvaa maski usoni kutasaidia watu kupata maambukizi, kuna ushahidi mdogo sana kuwa kitendea kazi hicho kinaweza kuwanufaisha watu wakiwa nje kwa sababu imebuniwa kwa ajili ya huduma za afya," anasema.

Anasema maski hizo kama hazikuvaliwa vizuri, kubadilishwa kila wakati kunaweza kuwa salama katika mazingira ya kazi.

Watu wangezingatia zaidi kufanya mazingira yao kuwa safi, kama hilo suala la usafi wangelipa kipaumbele, anasisitiza Dkt. Dunning.

**KWA MSAADA WA BBC**

## HABARI KIMATAIFA

# Mshirika wa Isabela apatikana amefariki

**LISBON,** Ureno

MFANYAKAZI mmoja wa benki anayehusishwa na kesi ya ufujaji wa ulanguzi wa fedha dhidi ya mwanamke tajiri barani Afrika, Isabel dos Santos amepatikana amefariki mjini Lisbon.

Nuno Ribeiro da Cunha mwenye umri wa miaka 45 alisimamia akaunti za kampuni ya mafuta Sonangol, ambaye mwenyekiti wake alikuwa Dos Santos katika benki ya EuroBic nchini Ureno.

Kifo chake kilitokea siku ya Jumatano na kuripotiwa Alhamisi muda mfupi tu baada ya waendesha mashtaka nchini Angola kuwataja wote wawili kama washukiwa.

Isabela amekana madai ya ufisadi yalifichuliwa na stakhabadhi zilizovuja.

**Vyombo vya habari nchini humo vilinukuu polisi wakisema Cunha alikuwa amejaribu kujiua mwezi huu na kwamba alikuwa akiugua shinikizo la akili.**

Bwana Da Cunha alipatikana amefariki katika mojawapo ya mali zake mjini Lisbon. Chanzo kimoja cha polisi kiliambia chombo cha habari cha Portugal kwamba huenda mshukiwa huyo alijiua.

Vyombo vya habari nchini humo vilinukuu polisi wakisema Cunha alikuwa amejaribu kujiua mwezi huu na kwamba alikuwa akiugua shinikizo la akili. Siku ya Jumatano Eurobic ilisema kwamba itasitisha uhusiano wake wa kibiashara na bi Dos Santos ambaye ameripotiwa kuwa mwanahisa mkuu wa benki hiyo kupitia kampuni mbili anazomiliki.

Baadaye iliripotiwa akisema kwamba mtoto wa aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo, Dos santoa atauza hisa zake katika benki hiyo.

Benki hiyo pia ilisema kwamba itachunguza uhamisho wa fedha usio wa kawaida unaohusisha makumi ya mamilioni ya madola ambayo zilikuwa katika akunti yake.

Baadhi ya fedha hizo zilifilisi akaunti ya Sonangol katika benki ya EuroBic kulingana na gazeti la New York Times.

Waendesha mashtaka wa Angola wanajaribu kukomboa dola bilioni 760m ambazo Isabela na washirika wake wanadaiwa kulipora taifa hilo.

Isabel dos Santos ametuhumiwa kwa usimamizi mbaya na ufujaji wa fedha wakati alipokuwa mwenyekiti wa Sonangol, alisema mwendesha mashtaka mkuu Helder Pitta Gros.

Alisema kwamba kutokana na hilo, atashtakiwa na ulanguzi wa fedha, kutumia ushawishi wake, usimamizi mbaya na kughushi stakhabadhi miongoni mwa uhalifu mwengine wa kiuchumi.

Mamlaka nchini Angola sasa itafanya uchunguzi ili kubaini iwapo atahitajika kushtakiwa. Pia wametaja watu wengine watano akiwemo bwana Ribeiro da Cunha na kuwataka kurudi nchini Angola.

Bwana Pitta Gros alisema kwamba iwapo Isabela hatorudi nchini humo mwenyewe, watatoa agizo la kimataifa la kumkamata. **BBC**

## Iraq waandamana kuipinga Marekani

**BAGHDAD,** Iraq

MAELFU ya raia wa Iraq jana wameandamana kwenye viunga vya mji mkuu, Baghdad, kuitikia wito wa kiongozi mashuhuri wa kidini wa kupinga uwepo wa vikosi vya jeshi la Marekani nchini humo.

Waandamanaji walipeperusha bendera za taifa na kupaza sauti za kaulimbiu za kuipinga Marekani, inayoongoza muungano wa kijeshi dhidi ya kundi linalojiita dola la kiislamu nchini Iraq na Syria.

Maandamano hayo yaliyoitishwa na Moqtada al Sadr yanalenga kuishinikiza Marekani kuondoa vikosi vyake vya jeshi kufuatia kuawa kwa Jenerali Qasem Soleimani wa jeshi la Iran na mkuu wa kundi la wanamgambo nchini Iraq.

Sadr anapinga uingiliaji wote wa kigeni nchini humo na hivi karibuni alijisogeza karibu na Iran ambayo washirika wake wanadhibiti taasisi muhimu za taifa tangu uvamizi wa Marekani nchini Iraq mwaka 2003. **DW**

## EU wakubali Uingereza kuondoka

**BERLIN,** Ujerumani

VIONGOZI wakuu wa Umoja wa Ulaya, jana wametia saini makubaliano ya mwisho ya kukamilisha mchakato wa Uingereza kujitoa kutoka umoja huo, Brexit.

Kutiwa saini mkataba huo na Rais wa Halmashauri kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen, na Rais wa Baraza Kuu la Umoja huo, Charles Michel, kutawezesha kuwasilishwa mbele ya Bunge la Ulaya Januari 29 ili kuidhinishwa.

Wanadiplomasia wanaowakilisha nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya wataridhia makubaliano hayo kwa maandishi ifikapo Alhamisi inayokuja kuwezesha Uingereza kutoka ndani ya umoja huo usiku wa manane wa Januari 31.

Akizungumzia hatua hiyo, Rais wa Baraza Kuu, Charles Michel, amesema licha ya kwamba mambo yatabadilika baada ya Brexit, lakini anajitayarisha kuukaribisha mwanzo mpya wa ushirikiano kati ya Umoja huo na Uingereza. **DW**



Mwanamgambo kutoka kundi la Jenerali Haftar akilinda moja ya eneo la Sirte kama alivyokutwa jana. **PICHA: AFP**

## China kujenga hospitali kutibu Corona

**BEIJING,** China

CHINA inaharakisha ujenzi wa hospitali mpya ndani ya muda wa siku 10 ili kuwatibu wagonjwa wa kirusi hatari cha Corona.

Hospitali hiyo inayojengwa kwenye mji wa Wuhan, ambako soko lake la samaki ndilo kitovu cha mripuko wa kirusi hicho, inatarajiwa kuwa tayari ifikapo Februari 3 mwaka huu.

Itakapokamilika itahudumia idadi ya wagonjwa inayoongezeka. Tayari watu 830 wameshaambukizwa kirusi hicho, huku 26 wakipoteza maisha na mamilioni wengine wamewekwa chini ya karantini katika juhudi za kujaribu kudhibiti kusambaa kwake.

Wakati huo huo, safari za ndege kati ya mji wa Moscow na Wuhan, zimesitishwa kutokana na wasiwasi wa kuenea kwa virusi vya Corona

Hayo yanajiri wakati taasisi inayoshughulikia chanjo na kinga za maradhi duniani imesema, chanjo dhidi ya kirusi hicho inaweza kupatikana katika kipindi cha mwaka mmoja unaokuja. **DW**

## Mataifa jirani na Libya yahimiza amani

**ALGIERS,** Algeria

MATAIFA yaliyo jirani na Libya yamelaani uingiliaji wa kigeni katika mzozo wa taifa hilo la Afrika Kaskazini, wakati wa mkutano mjini Algiers, Algeria.

Mkutano huo ulioandaliwa na nchi hiyo hapo juzi, uliwaleta pamoja mawaziri wa mambo ya kigeni kutoka Tunisia, Misri, Chad na Mali pamoja na wale wa mataifa ya Sudan na Niger.

Waziri wa mambo ya kigeni wa Ujerumani, Heiko Maas, pia alialikwa kwenye mkutano huo.

Washiriki walisisitiza umuhimu wa kuheshimu uhuru wa Libya na mipaka yake na kutoa wito kwa pande hasimu kutatua mzozo huo kwa njia za amani.

Mazungumzo ya mjini Algiers yamefanyika siku kadhaa tangu mkutano wa kimataifa juu ya Libya ulioitishwa mjini Berlin, ambako viongozi wa ulimwengu walikubaliana kuheshimiwa marufuku ya kuingiza silaha nchini humo. **DW**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 37

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

Na Adam Fungamwango

NADHANI nilikueleza kuwa hata mimi nilisimama juu yako, walitaka kukuua mle ndani ya jumba letu, lakini niliwaambia kuwa chochote mnachotaka kumfanya fanyeni, lakini msimuue au kumtesa kiasi cha kusababisha ulemavu au kutetereka kwa afya yake, la sivyo na mimi nitajiua, kitu ambacho marehemu mama hakutaka kabisa kitokee.

Taarifa ya siri nilipenyezewa kuwa kama nikikataa kuolewa basi watakutafuta wakuue kwa sababu walidhani kuwa wewe ndiyo unayesababisha mimi nikatae kuolewa, ndiyo iliyofanya mimi kuolewa bila kupenda kwa Dk.Kapilima ili kulinda uhai wako.

Tayari wao waliona kuwa mimi nakupenda na wewe nakupenda. Ni kweli Kadili hakukuwa na kitu kama hicho. Wala hakuna hata siku moja tuliopanga au kuambizana maneno ya mapenzi. Tuliogopana.

Lakini siku zote mapenzi ni hisia na si maneno. Penzi linaonekana zaidi kuliko kusikika. Muonekano wetu tu bila kuambiana ilionekana tunapendana. Na hata waliotuona waliona kabisa tunapendana. Lakini leo ndiyo unaniambia maneno hayo.

Na mimi nakuambia kuwa yale yote waliokuwa wakiyaona na kuhisi yalikuwa ni kweli. Na mimi pia nakupenda." Alisema Edina naye akijibu mapigo kutoka kwa Kadili.

"Hatujapendana leo, sema tu leo tumeambizana ukweli ulio moyoni mwetu, lakini tulipendana tangu zamani. Vitendo vyako na vyangu vilionekana kuwa tunapendana. Na yote yaliyotokea ni kwa sababu tunapenada. Umetesema kwa sababu unanipenda. Nimeteseka kwa sababu nakupenda. Niko hapa leo kwa sababu nakupenda." Alinong'ona Edina na machozi yalianza kumtoka. Alilia kwa kwikwi, lakini bila sauti.

Alijiegemeza kwenye mapaja ya Kadili. Pamoja na kwamba ametoka kwenye familia ya kitajiri na anakaribia kurithi mali na kampuni zote za marehemu mama yake, lakini bado alibaki kuwa ni mwanadamu na mtoto wa kike mwenye hisia kama mwingine yoyote yule.

Kwa muda mrefu alikuwa na funda moyoni mwake. Alimpenda Kadili licha ya umasikini wake. Alipambana bila kumwambia chochote. Lakini leo anamfunulia ukweli baada ya yeye kufunuliwa ya moyoni kutoka kwa mtu aliyempenda.

Kilikuwa ni kilio cha furaha. Kilio cha kukaribia kupata ushindi ulioonekana mgumu na wenye vikwazo.




**Edina kwa upande wake alimpenda Kadili tangu siku ile alipomuona kule disco, lakini mazingira ndiyo yaliyomfanya asiseme lolote, au kumuonyesha chochote Kadili kama anapendwa, badala yake alihakikisha tu anakuwa mzima na afya, akiomba Mungu pia hadi siku ambayo alijua itafika ili afunue ukweli.**

"Usilie Edina, nadhani sasa ni wakati wa furaha unawadia." Kadili alibembeleza.

"Niache nilie Kadili. Tena nilie sana. Nitoe machozi mengi tu. Waketi ule matatizo yalipokuwa yamepamba moto kwako na kwangu ilikuwa ni mateso. Nililia moyoni, machozi hayakutoka machoni. Yalikuwa hayatoki kwa sababu nilitaka kupambana kuhakikisha nakubakisha salama Kadili wangu. Leo naweza kusema kuwa uko hai, uko salama na pia vikwazo vyote vimekwisha, sasa ni wakatu wangu wa kulia. Ni wakati wa kuvuta picha na kumbukumbu zote tangu mwanzo hadi mwisho na kugundua kuwa ulikuwa kwenye hatari kubwa, lakini tumefanikisha kushinda mpenzi, cha tu nilie..." Alishindwa kuzungumza na kulia taratibu kwa kwikwi alimkumbatia mpenzi wake kwa nguvu.

"Edina nakuahidi nitakuona na nitakufanya uwe na furaha maisha yako yote."

****************************************

Chakula kililiwa na familia nzima. Hakikuwa rasmi kwa ajili ya mgeni kwa sababu alikuja kwa kushtukiza, lakini familia ilikula kwa furaha.

Kadili alikuwa na furaha kwa sababu kazi ngumu ilikuwa imekwisha. Amejipambanua kwa Edina na hata msichana mwenyewe naye amekubali kuwa naye.

Edina kwa upande wake alimpenda Kadili tangu siku ile alipomuona kule disco, lakini mazingira ndiyo yaliyomfanya asiseme lolote, au kumuonyesha chochote Kadili kama anapendwa, badala yake alihakikisha tu anakuwa mzima na afya, akiomba Mungu pia hadi siku ambayo alijua itafika ili afunue ukweli.

Hakujali umasikini wa Kadili kwa sababu hakuuhitaji, alichohitaji ni penzi tu, kwani tayari yeye ni ametoka kwenye ukoo wa kitajiri, hivyo haukumsumbua kichwa.

Tatizo lilikuwa ni mama yake na mitazamo ya watu wengine, lakini kwa sasa vikwazo vyote vimeondoka.

Mama Kadili alijua kila kitu. Tangu wakati ule kijana wake anakwenda disco na kupata umbea kuwa anapendana na binti wa kitajiri kutoka kwa mama Gombea.

Mambo yote yaliyotokea kati, ikiwemo kutekwa na kuteswa vibaya anatambua kila kitu na hata akampiga marufuku kijana wake kumfuatilia mwanamke huyo na kumwambia kuwa huyo si mwanamke ila muuaji.

Alijua kabisa kuwa tabaka ya umasikini na utajiri ndiyo unaokwamisha kijana wake, hivyo kuamua kukaa kikao cha kaka yake ili amtoe binti yake Eliza aolewe na Kadili, kwani sababu binti huyo naye anatisha kwa urembo.

Hicho ndicho alichokuwa akisubiri, lakini Kadili bado alikuwa akipiga chenga.

Leo hii amejionea kwa macho msichana aliyekuwa akimsumbua kijana wake. Anakula naye chakula. Binti wa kitajiri, mrembo, lakini amekuja kwake, kwenye kijumba kidogo, anaongea na kula kwa heshima zote.

Anayemheshimu kila mtu. Akatokea kumpenda tu ghafla. "Huyu msichana kweli anamfaa mwanangu." Aliwaza. Eliza aliyekuwa amekaa sambamba na Edina, pamoja na urembo alionao, lakini alikiri moyoni kuwa amekutana na kiboko yake.

Pamoja na hayo, aliona kabisa kuwa moyo na akili za Kadili siku zote zilikuwa kwa Edina na si yeye.

Ni kweli alikubali kuolewa na Kadili kama dili lilivyopangwa na baba yake mzazi na dada yake ambaye ni mama Kadili ili waoane mtu na dada yake binamu, lakini tangu afike pale, aliona dalili zote za Kadili kuwa haziko kwake, bali kwa binti huyo ambaye leo ndiyo amemuona kwa macho yake.

Kwa mbali furaha ilimjia kwani sasa atakuwa huru kuchagua mtu ampendaye na si kulazimishwa tena na familia kama ilivyotaka iwe.

Mgeni aliaga. Mama alimkumbatia mkwewe mtarajiwa. Machozi yaliwatoka.

"Sasa mama mimi hapa ni mwenyeji, hapa ni nyumbani kwangu." Edina alimwambia Mama Kadili.

"Karibu mwanangu."

Safari hiyo ilitoka hapo na kwenda kwa kina Meze. Edina alitaka ajue sehemu zote ambazo rafiki zake aliokuwa akikutana nao disco miaka kadhaa iliyopita.

Awali safari ilikuwa ni wa watu watatu, Kadili, Edina na Meze. Lakini safari hii aliongezeka mmoja.

Meze ambaye alirejea baadaye kuungana na familia ya rafiki yake kula chakula cha mchana, alikuwa alikuwa anatoka hapo na rafiki zake hao wawili, lakini akiongezeka Eliza.

Huko hakukaa sana na tayari giza lilikuwa limeshaingia, hivyo wenyeji wake watatu walimpeleka alipopaki gari lake.

"Kadili, Meze na shoga'angu Eliza, wiki ijayo nitakuwa na pati kubwa nyumbani linalohusu tukio hili lililotokea lao la kihistoria. Nitawaandaa sherehe fupi hivi, kwa hiyo mjiandae nakuja kuwachukua mimi mwenyewe." Alisema Edina na kuongeza.

"Hii pati mama haimhusu, itakuwa ni ya vijana tu kwa sasa sisi wenyewe, yeye mama nitakuja kumchukua siku nyingine aende akapajue nyumbani."

"Asante wifi yangu, wala usikonde." Alijibu Eliza.

Alipofungua mlango, kabla ya kuingia, alimtazama Kadili na kumkumbatia.

Wakati wakiwa na bahari ya mahaba, Kadili aligeuza kichwa nyuma yake.

Macho yake yaliwaona Meze na Eliza wakiwa wanawaangalia kwa tabasamu, halafu na wao wanatazama usoni.

**Itaendelea Jumamosi**

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanz MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;14/2020
Ombi la **ISSA ISUMAIRI HALIFA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ISSA ALIFA MOHAMED

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/01/2020.

215598802

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

HEMED HAMISI MPAGAMA amepotelewa na kadi ya pikipiki MOTOR TRICYCLE TVS KING yenye namba za usajili MC 712 BKY Ambaye mmiliki ni IBRAHIM ANDREW KINTOMA.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi.

Taarifa ya polisi: MOR/MOR/RB/76695/2020.

215598902

### KADI YA GARI IMEPOTEA

PETER STEVEN GAZIGILE

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Yenye Namba za usajili **T349 AHJ** Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae.

ARU/ARU/RB/77799/2020

215598702

### KUPOTEA KWA VYETI



**MWANAMKASI JUMA MLANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1633/0092** kilichotolewa na OLD TANGA SEKONDARI mwaka 2015. Result slip ya kidato cha sita yenye index namba S.2021/565 iliyotolewa na WERUWERU GIRLS SEKONDARI mwaka 2018. Pamoja na cheti cha kuzaliwa.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: DAR/KIG/RB/58289/2020.

215598101

### TANGAZO LA KUMBUKUMBU LA KIFO CHA BABA FAUSTINE PETER NYAKI.



Leo tarehe **25/1/2020** Baba yetu umetimiza miaka 20 tangu ulipoitwa na Mwenyezi Mungu.

Sisi kama familia yako tunakumbuka sana na tunaendelea kuyaenzi na kuyaishi yale yote. uliyotuachia kama busara, hekima, kumcha Mungu na kufanya kazi kwa bidii na maarifa.

**Basi itoshe kusema tu Baba endelea kupumzika kwa amani.**
**Amina**

115598202

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ELIAPENDAVYO CHARLES MSIGALO anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 406 ASK** aina ya **FEKON.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MKH/RB/526/2019.**

215598302


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MARQUINHOS NJE PSG WIKI TATU



**PARIS,** Ufaransa

BEKI wa klabu ya Paris Saint-Germain, Marquinhos atakuwa nje ya dimba kwa kipindi ch mwezi mmoja baada ya kuumia misuli ya nyama za paja, wakati wa mchezo wa ushindi wa Kombe la Coupe de la Ligue dhidi ya Reims.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazili alifunga bao la ufunguzi wakati PSG ikiibuka na ushindi wa 3-0 kwenye mchezo huo wa nusu fainali Jumatano, lakini alilazimika kuondoka dimbani zikiwa zimesalia dakika 20 mchezo kumalizika.

Anaonekana ataukosa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Lille, Montpellier, Nantes na Lyon, pamoja na mchezo wa raundi ya tatu wa Kombe la Coupe de France wiki ijayo dhidi ya Pau.

Katika taarifa ya PSG, ilitangaza: "Marquinhos ameumia misuli ya nyama za paja Jumatano kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Auguste Delaune na vipimo vinaonyesha hivyo.

# Hazard, Ramos warejea kikosini Real

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard amerudi kwenye mazoezi baada ya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu kutokana na majeruhi, huku pia Real Madrid wakimkaribisha Sergio Ramos ambaye amerudi kikosini.

Hazard alisajiliwa kutoka Chelsea Juni mwaka jana na aliukosa mwanzo wa msimu huu kwa majeraha ya misuli ya nyama za paja na amekuwa nje ya dimba tangu Novemba akisumbuliwa na matatizo ya 'enka'.

Mshambuliaji huyo amecheza mechi 13 tu katika mashindano yote kwa Los Blancos hao akifunga bao moja.

Hata hivyo, Hazard sasa amerudi na alikuwa kwenye mazoezi ya kikosi cha Madrid Alhamisi, na alionekana akikimbia na mpira na kupiga mashuti, kwa mujibu wa tovuti ya klabu hiyo.

Hata hivyo, Hazard ana nafasi finyu ya kuwa fiti kwa ajili ya mchezo wa Jumapili dhidi ya Real Valladolid, ingawa Madrid ina matumaini ya kumtumia mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji wakati watakapocheza na Atletico Madrid katika dimba la Santiago Bernabeu, Februari Mosi.





# *Moses atua mikononi mwa Conte*

**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan imetangaza kumsajili Victor Moses kutoka Chelsea kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 29, anajiunga na miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa kipindi cha msimu wote uliobaki baada ya kutumia nusu ya msimu akiwa na Fenerbahce kwenye Ligi Kuu ya Uturuki.

Moses alikuwa mchezaji nguzo chini ya Antonio Conte wakati Chelsea ikitwaa taji la Ligi Kuu ya England msimu wa 2016-17 na anajiunga na kocha wake wa zamani, Antonio Conte pale kwenye dimba la San Siro.

Inter haikuthibitisha kiasi cha fedha ambacho watalazimika kulipa wakati watakapomnunua moja kwa moja, lakini imeripotiwa kuwa watatakiwa kutoa kiasi cha euro milioni 10 ili kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Nigeria.

Moses ni mchezaji wa hivi karibuni kutoka Ligi Kuu ya England kutua hapo Inter, ambao wapo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Serie A, wakipitwa pointi nne na mabingwa Juventus.

Romelu Lukaku na Alexis Sanchez walijiunga na timu hiyo wakitokea Manchester United wakati wa dirisha lililopita la uhamsiho, kabla ya Ashley Young kuwafuata mwezi huu kweye kikosi hicho cha Nerazzurri.

Huku Moses akiwa tayari ametua hapo, Inter sasa wanatarajia kukamilisha jitihada zao za kumsajili Christian Eriksen, huku tayari wakiwa wametuma ofa yao kwa Tottenham wiki hii.

Moses anaweza kuanza kuichezea timu hiyo kwenye mchezo wa Serie A Jumapili dhidi ya Cagliari.

# Barcelona kuitibulia Inter kwa Eriksen

**LONDON,** England

BARCELONA imeulizia uwezekano wa kuipata saini ya Christian Eriksen kutoka Tottenham katika dirisha hili la usajili la Januari.

Eriksen alikutana na Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, Jumanne na kumweleza kwamba anataka kujiunga na Inter Milan mwezi huu, kwa mujibu wa Sky Sports Italia.

Inter bado inatoa msukumo mkubwa wa kumpata, lakini sasa inaonekana kama Barcelona ipo katika nafasi ya kuipata saini yake.

Hata hivyo, wakati bado kukiwa hakuna makubaliano kati ya Tottenham na Inter kuhusu hitimisho la ada ya uhamisho kwa Eriksen, malipo binafsi yanaaminika wameshakubaliana na dili hilo linakaribia kukamilika, kwa mujibu wa Sky Sports Italia.

Mkataba wa Eriksen unamalizika mwishoni mwa msimu na amekuwa huru kufanya mazungumzo ya awali na klabu zilizopo nje England tangu Januari Mosi, mwaka huu.

Jumatatu Inter ilitaka kutoa pauni milioni 11 pamoja na bonasi kwa nyota huyo wa kimataifa wa Denmark, lakini Spurs ikashikilia kuwa thamani yake ni pauni milioni 17.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta ana matumaini klabu hizo mbili zitafikia makubaliano katika dili hilo la Eriksen mwezi huu. Aliiambia Sky Sports Italia: "Eriksen ni mchezaji bora. Tunasubiri na bado tunaamini katika dili hili."






# SETIEN, VALVERDE HAWANA TOFAUTI, ASEMA DE JONG

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Frenkie de Jong amesema mbinu hazijabadilika sana tangu Quique Setien achukue nafasi ya kuwa kocha mkuu kutoka kwa Ernesto Valverde.

Valverde alifukuzwa baada ya kufungwa 3-2 na Atletico Madrid kwenye nusu fainali ya Supercopa de Espana, huku Setien - akianza kwa kutumia mbinu za Johan Cruyff za kumiliki zaidi mpira.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 61, staili yake ilionekana kuwa na matunda mazuri kwa Barca, kwa miamba hao wa Catalunya kuwa na umiliki wa asilimia 82.4 wa mpira kwenye mchezo wa ushindi wa LaLiga dhidi ya Granada na asilimia 78 kwenye mchezo wa ushindi wa Jumatano dhidi ya Ibiza katika Kombe la Mfalme ('Copa del Rey').

Barca imefunga mabao matatu tu kwenye mechi hizo mbili, ingawa bado hawajawa kwenye ubora wao katika safu ya ushambuliaji, kitu ambacho alikuwa akishutumiwa nacho Valverde mara kwa mara. Na De Jong amesema Setien bado hajafanya mabadiliko makubwa kwenye timu hiyo, akiwaambia waandishi wa habari Alhamisi.

"Hajasema chochote cha kiufundi kwa upande wangu. Ana mawazo sawa na Valverde, kwa staili ya umiliki wa mpira ya Barcelona.

"Kitu pekee ambacho kimebadilika ni maelezo machache, lakini malengo ni kuwa na mpira."

# *Podolski ajiunga na Antalyaspor ya Uturuki*

**ANKARA,** Uturuki

LUKAS Podolski amejiunga na klabu ya Antalyaspor inayojikongoja kwenye Ligi Kuu ya Uturuki, Super Lig, kwa uhamisho huru baada ya kuondoka Vissel Kobe.


Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani, Podolski alikuwa akicheza kule Vissel tangu mwaka 2017, akiwa amejiunga na klabu hiyo ya Japan akitokea Galatasaray na alikuwa akihusishwa na mabingwa wa Malaysia, Johor Darul Ta'zim baada ya kuwatembelea kwenye uwanja wao wa mazoezi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, badala yake akaamua kurudi nchini Uturuki na kujiunga na Antalyaspor, ambao walimaliza nafasi ya saba msimu uliopita, lakini sasa wapo kwenye mstari wa kushuka daraja baada ya kucheza mechi 18 msimu huu wa 2019-20.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na mshambuliaji wa zamani wa Arsenal na Bayern Munich, ambaye ataava jezi namba 11 kwa klabu yake hiyo mpya, pia alikuwa kwenye mazungumzo na Cologne.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MANE SASA AIPA PIGO LIVERPOOL

●●● Alilazimika kutoka nje, natumaini majeraha yake si mabaya sana, lakini tutaona...

**LIVERPOOL,** England

SADIO Mane ameumia misuli ya nyama za paja, lakini Liverpool bado haijajua tatizo hilo ni kubwa kwa kiasi gani, amesema kocha Jurgen Klopp.

Nyota huyo wa kimataifa wa Senegal alitolewa nje kipindi cha kwanza kwenye mchezo wa Ligi Kuu wa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Wolves, Alhamisi.

Mane aliumia wakati alipokuwa akikimbilia pasi ya Mohamed Salah na nafasi yake ilichukuliwa na Takumi Minamino dakika ya 33.

**Klopp ana matumaini majeruhi hayo hayatakuwa makubwa zaidi, lakini anasubiri kwanza kupata majibu ya vipimo alivyofanyiwa jana Ijumaa.**

"Sadio kwa hakika alilazimika kutoka nje," alisema akiiambia BBC Sport. "Natumaini, majeraha yake si mabaya sana, lakini tutaona kesho (jana)."

Klopp aliongeza kuwaambia waandishi wa habari: "Alihisi kitu fulani kwenye misuli ya nyama za paja. Hatujui bado tunatakiwa kusubiri."

Bao la kuongoza la Jordan Henderson lilisawazishwa na Raul Jimenez na Wolves walionekana kama wanaelekea kupata pointi moja waliyostahili kabla ya Roberto Firmino kufunga la ushindi dakika ya 84.

Klopp alikubali kikosi chake hakikuwa kwenye ubora, hasa bao la Wolves lilimchanganya, lakini alifurahishwa na lile la Firmino.

## ZISIKUPITE

### TEVEZ ANUKIA TENA UNITED

Manchester United inaweza kushtukiza kwa kwenda kumsajili kwa mara nyingine mshambuliaji Boca Juniors, Muargentina Carlos Tevez, 35. ***(Tuttosport)***

### LIVERPOOL YAJITOSA KWA ISCO

Liverpool inavutiwa kumsajili kiungo wa Real Madrid, Isco, 27, ingawa miamba hiyo ya La Liga inataka takriban pauni milioni 59 kwa nyota huyo wa kimataifa wa Hispania. ***(El Desmarque - in Spanish)***

### AIFUNGULIA BARCELONA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30, amefungua milango ya kujiunga na Barcelona. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### CHELSEA YAMRUDIA DEMBELE

Chelsea imefungua tena mazungumzo na Lyon kuhusu dili la kumsajili mshambuliaji Mfaransa Moussa Dembele, 23, mwezi huu endapo tu itamkosa straika wa Paris St-Germain, Edinson Cavani, 32. ***(Sun)***

### LEMAR ATAJWA ARSENAL

ARSENAL inapewa nafasi ya kumsajili kiungo Mfaransa Thomas Lemar, 24, kutoka Atletico Madrid. ***(Express)***

### FERNANDES BASI TENA UNITED

Manchester United imehitimisha mchakato wake wa kwenda kumsajili kiungo Bruno Fernandes kwa sababu wamekataa kufika dau la pauni milioni 68 ambazo Sporting Lisbon inahitaji ili kumwachia Mreno huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Mail)***

### ANCELOTTI AMTAKA HOJBJERG

KIUNGO wa Southampton, Mdenmark Pierre-Emile Hojbjerg, ni chaguo la kwanza kwa kocha wa Everton, Carlo Ancelotti katika dirisha hili la usajili. ***(Star)***

### CHELSEA, BARCA KWA ARIGONI

CHELSEA na Barcelona zinamfukuzia beki wa kushoto wa Grasshopper, Mswisi Alan Arigoni, 21. ***(Blick - in German)***

### VILLA YAKWAMA KWA SLIMANI

Leicester imeikataa ofa ya Aston Villa ya kumsajili Islam Slimani, 31, kwa mkopo kwa kipindi kilichobaki cha msimu. 'Mbwea' hao watazingatia tu ofa ya kumnunua jumla nyota huyo wa kimataifa wa Algeria, ambaye anacheza kwa mkopo Monaco. ***(L'Equipe, via Star)***

### LLORENTE KUMZUIA GIROUD

Inter Milan imefungua mazungumzo na Napoli ya dili la kumsajili straika Mhispania Fernando Llorente, mpango ambao utaishuhudia klabu hiyo ikihitimisha kuvutiwa kwake na mshambuliaji wa Chelsea. Mfasransa Olivier Giroud, 33. ***(Sky Sports)***

### NEWCASTLE YAMTAKA ROSE

Newcastle United ipo tayari kutoa ofa kwa beki wa Tottenham, Muingereza Danny Rose. ***(Evening Standard)***

### MADDISON BADO AITESA UTD

MANCHESTER United bado inaamini itamsajili kiungo wa Leicester City, Muingereza James Maddison. ***(Star)***

HABARI MICHEZO

## ZFF yatangaza kikosi Z'bar U-16

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIKOSI cha timu ya Vijana ya Zanzibar chini ya umri wa miaka 16, kimetangazwa kuelekea mchezo wao wa kirafiki dhidi ya timu ya Vijana ya umri huo kutoka Tanzania Bara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Mohmed Ali Hilali, alisema lengo la mchezo huo ni kuchagua wachezaji watakaounda timu ya Taifa ya Vijana ya Tanzania U-16 kuelekea michuano ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa U-16.

Alisema kikosi hicho kitacheza michezo miwili leo saa 10:00 alasiri katika Uwanja wa Amaan huku kikirejea tena uwanjani hapo Jumapili saa 2:00 asubuhi.

Hilali alisema kikosi hicho cha Zanzibar kitakuwa chini ya Mohmed Seif maarufu Kocha Kikngi

Akitangaza kikosi hicho mbele ya waandishi wa habari chenye wachezaji 29, Kocha Msaidizi wa timu hiyo ya Vijana, Mohmed Ali Mrashani, aliwataja makipa kuwa ni Haji Mshenga- (Wales), Juma Haji Makame (New power) na Omar Haidar Faki (Barcelona).

Mabeki aliwataja kuwa ni Mohmed Ali (Paris), Abdul Hamid Ali ( Paris), Abdul majid Jafar (Mapembeani), Haji Mmanga (Wales FC), Juma Mohmed (JKU Academy), Subet Amour (Mpira Pesa) na Yafii Abdu (Sprus).

Kwa upande wa viungo ni Mohmed Mwinchande (ZFCD), Is-haka Jumbe Sleiman (New City), Fahadi Khamis Machano (Stride City), Feisal Twahir (Mapembeani), Kassim Hassan (Haroun- SapSoap), Mundhir Abdul (Rahman - Annour), Suleiman Kidawa (Black Sailor), Abdulkadir Seif (Real Kids), Edward Emanuel (Mwambao FC), Abdurazak Yassir (Muembeni), Afllah Abdalla ( An Nour) nacRamadhani Mzee (Lion Muyuni).

Washambuliaji ni Salum Said ( ZFCD), Abdulrahman Khamis (Barcelona), Abdul Hafidh Kibobes (Mpira Pesa), Lukman Rashid (Black Sailor), Harith Ame (Black Lion) na Ali Abdallah (KMKM Academy)

## Mvua yazipeleka JKT, Tukuyu Uhuru

**Na Shufaa Lyimo**

MVUA iliyonyesha jijini Dar es Salaam juzi, imekwamisha mchezo wa Kombe la Shirikisho kati ya timu ya JKT Tanzania na Tukuyu Stars kutokana na Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo kujaa maji, hivyo sasa kuhamishiwa katika dimba la Uhuru leo saa nane mchana, imeelezwa.

Akizungumza jana, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Bahressa, alisema kikosi chake kipo vizuri kuelekea katika mchezo huo wa leo baada ya mvua kuupeperusha juzi.

Bahressa alisema hana wasiwasi na wachezaji wake kutokana na mbinu mbalimbali alizowapa ili kuibuka na ushindi na kisha kusonga mbele.

# AZAM FC YAJIPANGA KUTOIDHARAU RANGERS

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Azam FC wamesema wamejiandaa imara kuwakabili Friends Rangers katika mechi ya raundi ya nne ya michuano hiyo itakayochezwa keshokutwa, Jumatatu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche ameliambia gazeti hili mechi hiyo kwao ni sawa na fainali na wachezaji wamejiandaa kucheza katika kiwango cha juu.

Cheche alisema hawatawadharau wapinzani wao kwa sababu mashindano hayo hayana muda wa kujirekebisha kutokana na kuchezwa kwa mtindo wa mtoano.

**"Tumejiandaa kuendelea kupambana na kuendeleza kasi ya ushindi, kila mechi kwetu ni fainali, hakuna mechi ndogo, tunahitaji kushinda na kusonga mbele, michuano hii ni mikubwa na inayotoa nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa moja kwa moja," alisema Cheche.**

Nahodha Msaidizi wa Azam FC, Salum Aboubakar "Sure Boy" aliliambia gazeti hili wamejiandaa kuonyesha ubora wao na malengo yao ni kutetea taji hilo walalolishikilia.

Sure Boy alisema wachezaji wote wanafahamu umuhimu wa kupata ushindi katika mechi ya kesho ili kuhakikisha wanasonga mbele na kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa baada ya kupoteza Kombe la Mapinduzi walilokuwa pia wanalishikilia.

Mechi hiyo ya Azam na Friends Rangers ndio itakayokamilisha raundi ya nne ya michuano hiyo ya Kombe la FA ambayo hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**WALETENI HAO...**



Wachezaji wa timu ya Mwadui FC, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana, kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho (FA Cup) dhidi ya Simba utakaochezwa leo uwanjani hapo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Shime ataka bao la mapema Burundi*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI timu ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17, ikitarajia kushuka dimbani kuwakabili wenyeji wao Burundi katika mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia kwa vijana utakaochezwa leo mjini Bujumbura nchini Burundi, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Bakari Shime, ametoa neno la ushindi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime alisema kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na wachezaji wake wako tayari kwa kupambana kusaka ushindi.

Shime alisema anahitaji kuona wanaanza kupata bao la ugenini mapema ili kulinda ushindi wao walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa Januari 12, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Alisema ameyafanyia marekebisho makosa yote waliyoyabaini katika mchezo uliopita na wataingia uwanjani huku wakiwaheshimu wapinzani ambao watakuwa nyumbani kwao na wanaamini wataingia na mbinu tofauti.

"Hakuna mchezo wowote wa soka duniani ambao hauna makosa, hata kama timu yako imeshinda, tumefanyia kazi upungufu wetu ili kujiweka vizuri kuelekea mechi ya kesho (leo), tunaamini Burundi watakuja tofauti na hasa kwa sababu wanacheza nyumbani kwao," Shime alisema.

Mshambuliaji wa timu hiyo, Joyce Meshack, alisema wataingia uwanjani wakiwa na nguvu mpya na wakiamini ndio wanaanza kazi ya kuwaondoa Burundi.

"Tumejiandaa kuingia uwanjani kama ndio kwanza tunaanza kazi, hatutaki kuyafikiria matokeo ya mechi ya kwanza, tunaamini Burundi nao wataingia wamejipanga kutokana na makosa yetu, kikubwa tutapambana kuhakikisha tunapata pointi tatu," alisema Joyce.

Tanzania itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1, walioupata katika mechi ya kwanza na mshindi wa jumla wa mchezo huo atakutana na Uganda au Ethiopia katika hatua inayofuata.

Michezo
Jumamosi Januari 25, 2020
Nipashe




Mane sasa aipa pigo Liverpool

HABARI UK.30



Wachezaji wa Simba katika moja ya ushindi wa mechi zao la Ligi Kuu msimu huu. **PICHA: MAKTABA**

## Eymael aona kitu Yanga vs Prisons

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwasha moto kwenye Ligi Kuu kwa kupata ushindi wake wa kwanza tangu aanze kuinoa Yanga, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mbelgiji Luc Eymael atakuwa na kibarua kingine kikali dhidi ya 'Wagumu' Tanzania Prisons kesho.

Yanga itaikaribisha Tanzania Prisons katika Uwanja wa Taifa kwenye mechi ya raundi ya nne ya Kombe la Shirikisho (FA Cup) ikitoka kuichapa Singida United mabao 3-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupoteza mechi mbili mfululizo ikiwa chini ya Eymael.

Tayari Eymael ameeleza ni mwenye furaha na kikosi hicho na anakunwa na ubora wa wachezaji hao ambao ameeleza kuona kitu cha kipekee kutoka kwao.

Hata hivyo, Yanga itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 wakati timu hizo zilipokutana kwenye Ligi Kuu katika Uwanja wa Samora mjini Iringa, lakini wakati huo kikosi hicho kikiwa chini ya Boniface Mkwasa.

Eymael alisema wachezaji wake wana kitu cha kipekee wakiwa uwanjani na hufurahia kuona wanavyopambana na kwamba ni wakati wao wa kuendelea kupambana na kupata matokeo chanya.

Mechi nyingine zitakazopigwa leo, Namungo itawavaa Biashara United huku Stand United ikiwafuata Majimaji na Lipuli ikiwaalika Kitayosa FC.

# SIMBA YAISHITUA DUNIA, BARCA, REAL ZAONGOZA

**Na Somoe Ng'itu**

### ●●● Yaipiku Hull City ya England na Rangers ya Scotland, Kocha Sven yeye aigeukia Mwadui akisema...

WAKATI Simba leo ikishuka Uwanja wa Taifa kuivaa Mwadui FC katika mchezo wa raundi ya nne ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (FA Cup), imeishtua dunia baada ya kuingia kwa mara ya kwanza katika orodha ya klabu zinazoongoza duniani kwa kuwa na wafuasi wengi kwenye mitandao ya kijamii.

**Kwa mujibu wa Mtandao unaojihusisha na utoaji wa takwimu na fursa za kimtandao kwa wanamichezo, klabu na mashirikisho wa Result Sports wenye makao makuu yake mjini Budingen nchini Ujerumani, umetoa orodha ya klabu za soka zenye wafuasi wengi duniani katika mitandao ya kijamii ambapo Simba inashika nafasi 151 huku ikizipita klabu kama Rangers FC ya Scotland iliyopo nafasi 153 na Hull City ya England nafasi ya 155.**

Katika orodha hiyo iliyotolewa Januari mwaka huu, Barcelona ndiyo kinara duniani ikiwa na wafuasi zaidi ya milioni 260 kutoka katika mitandao yake ya Instagram, Twitter, Facebook, YouTube na milioni nane katika mitandao mingine.

Real Madrid inafuata ikiwa na wafuasi zaidi ya milioni 258, Manchester United (milioni 142) ikishika namba tatu huku Chelsea yenye wafuasi milioni 93 ikiwa nafasi ya nne Juventus (miloni 90), nafasi ya sita, Bayern Munich (milioni 83), Liverpool (milioni 83), Paris Saint-Germain (milioni 79), Manchester City (milioni 79) na Arsenal (milioni 77) ikifunga orodha ya 10 bora.

Kwa upande wa klabu za Afrika, mabingwa mara nane wa michuano ya Klabu Bingwa Afrika, Al Ahly wanaongoza kwa wafuasi wengi ikiwa na zaidi ya wafuasi milioni 25, ikishika namba 18 duniani. Nafasi ya pili kwa Afrika inafuatiwa na Zamalek yenye wafuasi zaidi ya milioni 11 huku ikishika nafasi ya 32 duniani.

Kwa Ukanda wa Afrika Mashariki klabu ya Simba inaongoza ikiingia kwa mara ya kwanza katika orodha hiyo, baada ya kushika nafasi ya 151 duniani huku ikiwa na wafuasi zaidi ya milioni moja. Facabook ina wafuasi zaidi ya 568,000, Instagram wafuasi zaidi ya milioni moja, Twitter wafuasi takriban 142,000 na YouTube ikiwa na wafuasi zaidi ya 21,000.

Tukirejea katika mechi ya leo, Simba itakuwa na kibarua kigumu itakapowavaa 'Wababe wao' Mwadui FC ambao mara ya mwisho kukutana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, mabingwa hao watetezi, Wekundu wa Msimbazi walikubali kipigo cha bao 1-0, mchezo ukipigwa Oktoba 30, mwaka jana kwenye Uwanja wa CCM Kambarage.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, alisema mechi zote wanazocheza ni ngumu na kuelekea mchezo huo, wamejiandaa kukabiliana na ushindani.

Sven alisema wamejiandaa kupambana katika dakika zote za mchezo huo ili kupata matokeo mazuri na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wako tayari kupeperusha vema bendera ya Simba na kutimiza malengo ya kushinda taji hilo linaloshikiliwa na Azam FC ya jijini Dar es Salaam.

"Tuko tayari kwa mechi, najua mechi itakuwa na ushindani, tunacheza na timu pekee iliyotufunga, lakini sasa kikosi kimeimarika zaidi na kimeongeza nguvu katika benchi la ufundi, natumaini tutafanya vizuri," alisema kocha huyo.

Kocha wa Mwadui FC, Khalid Adam yeye aliliambia Nipashe kuwa wamekuja jijini kwa kazi moja ya kusaka ushindi ili wasonge mbele katika michuano hiyo.

Adam alisema wataingia uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao na kubwa wakiheshimu ubora wa kikosi cha vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Utulivu na kutumia vizuri nafasi tutakazotengeneza, haitakuwa na maana kama tutapoteza mipira na nafasi tutakazopata, kikubwa tumekuja kutafuta ushindi ili tusonge mbele, " Adam aliongeza.

Mechi nyingine za mashindano hayo zitakazochezwa leo ni Mtibwa Sugar dhidi ya Sahare FC, Ndanda FC vs Dodoma FC, Gwambina vs Ruvu Shooting, African Sports vs Alliance FC, Ihefu vs Gipco FC, JKT Tanzania vs Tukuyu Stars na Kagera Sugar watawakaribisha Might Elephant.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >